**KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI KARATASI 1**
**INSHA**
**MUDA: SAA 13/4**

1. **LAZIMA**
   Mwandikie barua mhariri wa Gazeti la Baraka ukimweleza sababu za watoto wengi katika kaunti yako kuacha shule na kujiingiza katika ajira za mapema.

2. Vipakatalishi vimeleta manufaa mengi nchini .
   Fafanua.

3. Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali:\
   Mcheka kilema hafi bila kumpata.

4. Andika kisa kitakachoanzia kwa maneno yafuatayo:
   Kushoto kulikuwa na jitu la miraba minne ambalo lilitema cheche za matusi ungedhania ni karakana …

**KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL**
**102/2**
**KISWAHILI KARATASI YA PILI**
**LUGHA**

**SEHEMU YA A: UFAHAMU** **(alama 15)**

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali*

"Swala la idadi kubwa ya watoto wadogo wanaoendelea kumiminika mijini na kuonekana wakiranaranda mijini ovyo,halijapewa umuhimu wowote wa haja na serikali za nchi nyingi,licha ya mijadala katika warsha anuwai,zilizofanyika kujadili swala hili nyeti.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Kwa kutokuwa na sheria ama sera iliyo wazi kuhusu haki na usalama wa watoto,sarikali zetu hazina budi kukubali kubeba uzito wote wa lawama. Hii ni kwa sababu, serikali zetu zimelipuuza na kuvalia miwani swala hili kwa kuchukulia kuwa litapotea lenyewe katika hewa yabisi. Yafaa ifahamike kuwa usalama wetu katika siku zijazo utategemea jinsi tutakavyolikabili ana kwa ana tatizo hili wakati huu. Wakati wa kutenda ni sasa. Aidha, watoto hawa wanaokulia mitaani bila malezi,maelekezo wala mwongozo mwafaka wa kimaisha, wanakua bila mapenzi hivyo hawajui maana ya kupenda. Wanachokijua ni chuki na haja ya kulipiza kisasi didhi ya jamii iliyowachonga jinsi walivyo.  Hawajali lolote hata kifo. Wako tayari kujikabidhi kwa haini yeyote mwenye nia mbaya,bila kujali matokeo, muradi tu, wapate riziki.

Tunapendekeza kwa serikali, washika dau kama vile mashirika ya kujitolea, viongozi wa dini, shule, vyuo na wananchi kwa jumla wachange bia katika kutafuta mikakati ya kulitatua tatizo hili kabla halijageuka kuwa janga la kijamii ambalo tutashindwa kulimudu. Mpango wa vijana hawa kujiunga na huduma ya taifa ni jambo linalofaa kutiliwa maanani.

Tunapendekeza makao Zaidi ya watoto wanaozurura mijini yajengwe ambapo watapata mafunzo ya kiufundi yatakayowawezesha kujitegemea maishani. Badala ya kulitegea mgongo swala hili, serikali zinawajibika kuwasajili hawa watoto ili waweze kuunganishwa na familia na koo zao.  Utafiti uliofanywa na wataalamu wa Elimu jamii umebainisha kuwa ni asilimia kumi tu ya watoto hawa wa mitaani wasiokuwa na mahali wawezapo kupaita nyumbani.  Asilimia tisini iliyobaki, angalau wana mahali wanapoweza kupaita nyumbani ilhali wanaendelea kuwa mitaani. Wazazi tumesahau wajibu wetu.  Wengi wetu tumelikimbia jukumu la ulezi tulilopewa na muumba.  Hawa waliojipaka masizi mwilin mzima, wanaozurura ovyo mitaani, si matokeo ya maumbile;hawakuja duniani kwa sadfa, hawakuulizwa wala kushauriwa.  Makosa ni yetu wazazi.  Tuliwaleta hapa duniani, kisha tukawakimbia.Hatutasamehewa duniani na akhera.

Mwenye njaa hana miiko. Ili kijiruzuku, hawa watoto daima wanachumia jaani.Kwa kudura ya jalia, huenda siku moja watalia kivulini.  Asiyekuwa na wake ana mungu.Aghalabu, watoto wanaozurura mitaani hupewa pesa na wafadhili.  Wakati mwingine wanaiba. Maisha haya ya kuomba au kuiba wanaona yanaridhisha Zaidi kuliko kumenyeka na kazi ya kibarua kutwa kucha. Kwa bahati mbaya, watoto hawa wamatumia pesa wanazopata kutoka kwa wafadhili kujichimbia kaburi.  Aidha pesa wanazopatiwa watoto hawa wanazitumia kununulia gundi badala ya chakula.

Wafadhili wanashauriwa wawape chakula hawa watoto badala ya pesa taslimu. Kusema kweli, unapompa mtoto wa mitaani pesa,utakuwa unainua biashara ya mwenye kiwanda cha gundi,jambo ambalo litakuwa sawa na kuweka sahihi mkataba wa kifo cha mtoto mwenyewe.

Wataalamu wa afya wanaonya kuwa gundi ikivutwa kwa muda mrefu inaweza kusababisha upofu au kifo.Wataalamu hawa wanazidi kutuarifu kuwa matumizi ya muda mrefu ya gundi huathiri ubongo,figo na maini. Mtumiaji pia anaweza kupoteza uwezo wa kutembea na hata kupooza kabisa.

Sababu wanazotoa hawa watoto ni kwamba, uvutaji gundi,huwaondolea njaa,baridi ya usiku na kuwatuliza mawazo. Ni jambo la kusikitisha kwamba tunaendelea kushuhudia bila kujali hawa watoto ambao ni kiungo cha jamii yetu,wakijiangamiza. Wananchi kwa ujumla hawaha budi kuhamasishwa dhidhi ya athari ya matumizi ya gundi.Wafanya biashara wanaowauzia watoto hawa gundi yafaa wakome,la sivyo wachukuliwe hatua.Kutolitatua tatizo hili la watoto wa mitaani hivi sasa,kutapeleka kuwako kwa kizazi cha mitaani ambacho kitazaliwa mitaani,kulelewa mitaani,kuoa mitaani na kufia mitaani.Kadiri mataifa yanavyoendelea kujitia hamnazo kuhusiana na swala hili,ndivyo tunavyokubalia jinai itawale,sasa na wakati ujao.

Hawa watoto watakapokua,watageuka kuwa wapigaji watu kabari,majambazi,wezi wa kutumia nguvu ama watatumiwa na mahaini kutimiza uhaini wao.Hawa watoto wenye njaa,watalazimika hatimaye,kuwatoa wenywe shibe tonge mdomoni.Matokeo ya hali hii ni kwamba katika siku zijazo,hawa ndio watu watakaotunyima starehe ya kulala unono.Watatuchafya mitaani,majumbani,vijijini na kutuvizia mabarabarani.Tuna sababu nzuri ya kutiwa hofu na tatizo hili,kwani jinsi kizazi kinavyozidi kupanuka,inaonekana tumelitega bomu ambalo litakuja kutulipukia usoni mwetu."

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Taja jambo moja linalochangia kuweko kwa watoto wanaorandaranda mitaani. (alama 1)

(b) Maisha ya mitaani huathirije watoto? ( alama 3)

(c) Tatizo la watoto wanaorandaranda mitaani laweza kutatuliwaje? (alama 3)

(d) Eleza maana ya: (alama 2)

  i) Hawa watoto wanachumia jaani
  
  ii) Jinsi kizazi cha mitaani kinavyozidi kupanuka,inaonekana tumelitega bomu ambalo litakuja kutulipukia usoni mwetu. (alama 2)
  
  iii) Mwenye njaa hana miiko. (alama 2)

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye taaria: (alama 2)

  i. Aidha:
  
  ii. Gundi:

**2. UFUPISHO:(ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo**

Lugha ndio msingi wa maandishi yote. Bila lugha hakuna maandishi. Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ni anina ya lugha ya masungumzo.

Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza kama vila michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa. Haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha. Ujuzi wa kila siku utasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile

ilivyo. Vilevile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amefiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati juao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambae amepatikana na mambo kama huyo hana budi kufahamu zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi. Fauka ya hayo , karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.

Inambidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza . Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.

a) Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65 (alama 10, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Jibu

b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho (Maneno 30) (alama 5 utiririko)

Matayarisho

Jibu

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Toa mifano miwili miwili ya (al.2)

i) Sauti ghuna ambazo ni vipasuo …………………………………….

ii) Sauti sighuna ambazo ni vikwamizo ……………………………….…………

(b) Onyehsa mofimu katika neno Aliyemcha (al.2)

(c) Andika sentensi yenye muundo ufuatao (al.2)

KN(W+V) + KT (t +RH)

(d) Tumia neno shirika kama nomino na kama kielezi katika kutunga sentensi moja (al.2)

(e) Kwa kutunga sentensi vumisha nomino nguruwe kuwa kivumishi cha idadi bainifu. (al.1)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kutendewa (al.1)

Mtoto wa waziri amekufa

(g) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi (al.2)

Msomi hakutuzwa siku hiyo

(h) Tunga sentensi moja inayobainisha maana mbili tofauti za neno chuma (al.2)

(i) Tambua kiima na aina za yambwa katika sentensi ifuatayo. (al.4)

Mwalimu mkuu hupigiwa nguo pasi na Maria

(j) Kwa kutumia mifano mwafaka fafanua miundo yoyote miwili ya kirai nomino (al.2)

(k) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi (al.2)

Mgeni huyo na mwingine walikula wali kwa uma

(l) Andika neno lenye silabi funge yenye muundo wa konsonanti moja (al.1)

(m) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika udogo wingi (al.2)

Ng'ombe wangu ana ndama mdogo

(n) Tunga sentensi zenye mipangilio ifuatayo; (al.4)

i) Kishazi tegemezi na kishazi huru

ii) Kishazi tegemezi na kishazi tegemezi

(o) Eleza matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo: (al.3)

Nyamunga na kitoto wamekuwa wakila, wakiimba kikasuku

(p) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi. (al.4)

Mtoto wa mjomba alikuja kwetu nyumbani jana

(q) Andika kwa msemo wa taarifa. (al.2)

'Yafaa tumwendee mama mkubwa ili atushauri juu ya jambo hili,' Amina alipendekeza.

(r) Andika kinyume cha: (al.1)

Chakula hiki kitamu nitakimeza

(s) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo. (al.2)

(i) Kiwakilishi nafsi huru

(ii) Kiwakilishi nafsi kiambata

4. **ISIMUJAMII (alama10)**

(a) Tofautisha kati ya kuhamisha msimbo na kuchanganya msimbo. (alama 2)

(b) Taja mambo mawili yanayochangia katika uhamishaji msimbo. (alama 2)

(c ) Taja kaida mbili zinazotawala maamkizi katika jamii huku ukitoa mifano mwafaka. (alama2)

(d) Fananisha sifa zozote nne za sajili ya maabadini na mahakamani. (alama 4)

**KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL**
**102/3**
**KISWAHILI KARATASI 3**
**FASIHI**

**SEHEMU YA A: TAMTHILIA**
**P.Kea:Kigogo**

**1. Lazima**

(a) Jadili jinsi kumi ambazo maudhui ya ukatili yanajitokeza katika Tamthilia ya Kigogo (alama 10)

(b) Eleza mifano kumi ya matumizi ya kinaya katika Tamthilia ya Kigogo. (alama 10)

**SEHEMU YA B**
**RIWAYA: CHOZI LA HERI**
(Assumpta K. Matei)
Jibu swali la Pili au la Tatu

2. "Watu husema kuwa binadamu hawawi sawa ila kifoni…"

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alalama 4)

b) Tambua mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)

c) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya. (alama 6)

d) Thibitisha kuwa hakuna usawa baina ya wanadamu. (alama 8)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**Au**

3. Jadili nafasi ya sehemu zifuatazo katika riwaya ya Chozi la Heri:

(a) Hotuba (alama 10)

(b) Uozo katika jamii (alama 10)

**SEHEMU C**
**HADITHI FUPI**
(Mtihani wa maisha)
'Leo mwalimu mkuu atajua kwamba mdharao biu hubiuka'

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)

(b) Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika mktadha huu. (Alama 6)

(c) Eleza wasifu wa mzungumzaji wa maneno haya. (Alama 2)

(d) Jadili maudhui ya elimu kama yanavyojitokeza katika hadithi hii. (Alama 8)

(Ndoto ya mashaka (Ali Abdulla)

**(5)** 'Kusema kweli lakini hata mimi sikuwa na nadhari katika kumpenda msichana huyu … Nilimpenda kufa! Lakini! Kwao bure tu!'

(a) Eleza mkutadha huu. (Alama 4)

(b) Taja mtindo wa lugha uliotumika katika mkutadha huu. (Alama 4)

(c) Taja sifa mbili za mzungumzaji. (Alama 2)

(d) Onyesha maudhui ya umaskini katika hadithi fupi ya Ndoto ya mashaka.

**SEHEMU YA D**
**USHAIRI**
**Jibu swali 6 au 7**

(6) **USHAIRI**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Daima alfajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu;
Ni miti yote hujipinda migongo
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Akichekelea ha ha ha ha ha ha ha …
Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho;
Kuna jambo gani linamridhisha?
Kama si kujua ni kutokujua
Laiti angalijua, laiti angalijua!

(a) Eleza matatizo manne yanayompata mzungumziwa. (Alama 4)
(b) Eleza mtindo wa lugha uliotumiwa na mshairi na utoe mifano. (Alama 8)
(c) Taja nafsineni katika shairi hili. (Alama 1)
(d) Eleza toni ya shairi hili. (Alama 1 )
(e) Taja mbinu mbili za uhuru wa kishairi uliotumika na utoe mifano. ( Alama 2)
(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

**(7) Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili

Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ila ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili.

Vingekuwepop viraka, kuutia, ngeushuruti mwili
Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili
Upya ukaungilika, kuvutia, roho na wake mwili.

Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
Sihofu kupata mawi, sitajua, kupigania mwili
Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili.

Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika, damu, jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili.

(a) Liweke shairi hili katika bahari tatu. (Alama 3)
(b) Eleza dhamira ya mshairi. (Alama 2)
(c) Eleza muundo wa shairi hili. (Alama 4)
(d) Toa mifano ya uhuru wa kishairi uliotumika. ( Alama 4)
(e) Eleza kwa kifupi maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (Alama 3)
(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D**
**FASIHI SIMULIZI**

A (i) Miviga ni nini? (Alama 2)
(ii) Eleza sifa nane za miviga. (Alama 8)

B (i) Ulumbi ni nini? (Alama 2)
(ii) Eleza sifa nane za ulumbi (Alama 8)

**KIGUMO CLUSTER**
**102/1**
**KISWAHILI KARATASI YA 1**
**INSHA**

1. **Lazima**
   Andika barua kwa mhariri wa gazeti la mzalendo ukieleza athari za mabadiliko ya tabianchi na upendekeze namna ya kukabiliana na hali hii

2. Andika kuhusu umuhimu wa vijana katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo.
   Bahati ni chudi

4. Tunga kisa kitakachokamilika kwa kauli ifuatayo:
   "…niliipapia ile bilauri ya maji kwa pupa. Sikuwa na uhakika kuwa kiu yangu ingekatika. Nikapiga mafunda mawili, matatu. Baada ya kugumia bilauri yote, ndipo nilipotambua kuwa kweli maji ni uhai."

**KIGUMO CLUSTER**
**CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA SEKONDARI**
**102/2**
**KIDATO CHA NNE**
**JARIBIO LA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2021**

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kwa makini kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Katika ofisi yake moja alimfuma mpiga taipu akimwambia karani mwingine, "... kamnyoa yule yatima shilingi zake elfu mbili maskini..." Lakini maongezi yalikatika kwa kutokeza Salma, na Salma hakutaka kuambiwa nani 'kinyozi'.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

"Yupo?" aliuliza.

"Ke -keshaondoka, bibi," alibabaika mpiga taipu,

"Kaelekea ofisi ya kati."

Salma naye alielekea ofisi ya kati. Huko pia mlango wa ofisi yake aliukuta umefungwa, na watu kadha wakimsubiri nje.

"Ameitwa na Mheshimiwa Waziri, tafadhali kaa umsubiri bibi," mwandishi alimwambia Salma, na Salma akapweteka juu ya kiti pamoja na wengine kumsubiri Karim.

"Je, umesikia mambo hayo?" Sauti ilinong'ona karibu na Salma, miongoni mwa watu waliokuwa wakisubiri na kumfanya Salma, atege sikio. "Usifanye mzaha, mjomba wangu kafutwa shilingi mia nane ndipo alipopewa waraka wa nyumba yake. Mzee mmoja jirani yangu kasumbuliwa we-e-e, hata na **kutahamaki** kupanguswa haki yake yote. Na wangapi! Na wangapi! Basi na weye jihadhari."

"Yatakwisha hayo! Hoja umoja wetu," mtu mmoja alieleza.

"A-a-a! Na hawa wanaodhulumiwa haki zao hufanyaje?" Sauti nyingine iliuliza.

"Wanalo?" Ilijibiwa. "Labda humjui mtu huyu weye. Mkuu wa Polisi nduguye kwa baba na **pangu pakavu** atapita wapi...?"

"Hakuna pa kupita," Salma alijibu rohoni mwake, yeye akiwa ndiye mwenye kumjua kuliko wote.

Hali kadhalika, Salma alijua kuwa pengine Karim hatarejea siku ile, na hata angerejea kauli yake isimgerudi nyuma. Akiwaacha wale watu wakijadili juu ya haja iliyopo ya mabadiliko kwa nchi nzima iliyojaa dhuluma, Salma aliona afadhali aende tena kwa mama yake akamjaribu, ingawa tama haikuwapo.

Alipoingia Mbiju na gari lake jekundu, alimkuta mamake na birika mkononi akitilia maji bustani yake ya maua, kavaa kanzu nyeupe, ya kukokota, rangi ya bahari. Alionesha mtu mzima tena, ingawa umaridadi ulimpa nuru.

"Karibu," alisema huku akizungusha birika katika shina la mwasumini. "Leo pia hukumleta Karim."

"Kashughulika na makazi yake," Salma alisema, mkono wake mmoja mfukoni na mwingine kashika mkoba wake uliokuwa ukining'inia chini ya ukwapa.

"**Haijambo wewe unanikumbuka kuliko Samir huko Ulaya.** Hupita miezi sita hajaniletea barua, na anapoleta huwa kashikwa na haja. Hiyo huko ndani ya barua yake, nimeipata jana, anataka shilingi elfu kumi. Ikiwa barua zenyewe za kutaka mapesa tu amhonge huyo kafiri wake wa Kizungu, afadhali asiniletee," Bibi Adili alisema huku akikung'uta birika tupu chini ya shina la mwaridi. Laiti angelizikata yeye mwenyewe ningempelekea japo

nusu yake, lakini haja hizo zimeanza tangu kupambana na huyo kafiri wa Kizungu, anazitaka amhonge Mzungu wake, na sisi atufanye mahayawani kama yeye. Sipeleki hata senti moja"
Salma ambaye hapo kabla hakuwa na tamaa ya kupata mradi wake, sasa alivunja moyo kabisa kabisa kwa maneno ya mama yake. Salma mwana mpenzi kuliko wote, atanyimwa alichotaka, seuze yeye Salma ambaye miezi miwili iliyopita alipewa shilingi elfu tatu.
*(Unukuzi kutoka Nyota ya Rehema, S.A Mohamed)*

a) Kwa kurejelea muktadha wa ofisini, fafanua aina sita za mabadiliko yaliyohitajika nchini kwa mujibu wa masimulizi haya. (alama 6)
b) Thibitisha kwamba Salma hakuwa mgeni katika ofisi ya kwanza aliyozuru. (alama 4)
c) 'Haijambo wewe unanikumbuka **kuliko** Samir'
Fafanua jinsi kauli hii haikuwa na ukweli kwa kumrejelea Salma. (alama 1)
d) Taja mambo mawili yaliyomkatisha tamaa Salma kuhusu ufanisi wa ombi aliloendea kwa mama yake. (alama 2)
e) Kwa kuzingatia maana zilizo katika kifungu, andika **vinyume** vya matumizi ya lugha yafuatayo. (alama 2)
   i) kutahamaki ………………………………………………………………………......
   ii) pangu pakavu…………………………………………………………………………

**2. UFUPISHO (alama 15)**

Mikopo ni njia mojawapo inayotumiwa na watu wengi kwa lengo la kujiendeleza na kujikuza kiuchumi na kwa hivyo kukopa ni jambo lisilokwepeka. Mikopo inakubalika katika mataifa yote ya ulimwenguni na kwa sababu hiyo, mathalani, serikali nyingi hurasimisha ardhi za wananchi kwa ajili ya kutumika katika kukopa kutoka kwenye taasisi rasmi. Kutokana na uzoefu, na labda urahisi wa namna fulani, watu wengi hupendelea mikopo isiyo rasmi inayopatikana kwenye mikoba na vikundi vya ushirika vya kuweka na kukopa.

Ikumbukwe kwamba haiwezekani kupata mkopo wa pesa kutoka kwenye taasisi rasmi bila kulipa deni. Ili kuonyesha uaminifu wake na uhakika wa kurejesha fedha za wenyewe, mkopaji hulazimika kuweka rehani nyumba, hatimiliki ya ardhi, mshahara wake kama yuko kwenye ajira rasmi au mali yake nyingine yoyote kama gari. Hii huwa ndiyo dhamana ya mkopo wake. Dhamana hii husimama kama mbadala wa mkopo ili kulipia deni taraa mkopaji atashindwa kurudisha fedha alizokopa.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Watu wanaokopa mikopo wanaweza kukumbwa na hatari mbalimbali kutokana na kulemewa na kulipa madeni yao. Kushindwa kusimamia biashara au miradi wanayoanzisha kwa mikopo hiyo ni miongoni mwa hatari hizo. Wanaoshindwa kudhibiti biashara au miradi yao hukosa kupata fedha za kulipia madeni yao kwa sababu ya kuhasirika.

Aidha baadhi ya wakopaji huwekeza kwenye miradi isiyozalisha faida na kwa hivyo mtaji wao unamomonyoka na hata kumalizika kabisa na kwa hivyo wanapata hasara mara mbili ya kupoteza mtaji ambao ni mkopo na kukosa fedha za kulipia mkopo wao. Kuna baadhi ya watu wanaoomba mikopo na kwenda kuitumia katika anasa na sherehe na kuishia kufilisika. Hawa ni wakopaji ambao hukopa bila mipango. Ole wao wanaoomba kwa njia hii!

Kadhalika hatari nyingine ya kukosa kulipa madeni ni kwamba mali iliyowekwa rehani inaishia kwa mauzo ya kupigwa mnada. Aghalabu, hii inapotokea, wanaoathirika moja kwa moja ni wakopaji, familia zao, wafanyikazi na jamii inayomtegemea mkopaji.

Kuna haja ya kutafuta namna ya kuwanusuru wakopaji kutokana na adha hii. Wakopaji wanafaa kushirikishwa katika namma bora za kutumia fedha za mkopo kwa ajili ya uwekezaji endelevu. Vilevile, wanafaa kuelimishwa kuhusu mbinu za kulipia madeni ili waepuke kufilisika. Kwa mfano, wanaweza kushauriwa waanze kulipa mikopo mara tu biashara yao inapoanza kushika japo kidogo kidogo ilmuradi bandu bandu huisha gogo.

Baadhi ya wakopaji hushindwa kulipa madeni kwa sababu ya kukopa mikopo mikubwa sana kuliko uwezo wao wa kulipa. Hawa ndio wanaostahili kutathminiwa kwa kina kabla ya mikopo yao kuidhinishwa kama njia mojawapo ya kuwaepusha kujiingiza katika jinamizi la kushindwa kulipa madeni. Waama, baadhi ya mashirika ya kifedha hutoa mikopo kwa awamu kama namna ya kuwadhibiti wakopaji wasibadhiri fedha za mkopo. Imedbibitishwa kwamba mbinu hii imewafaa baadhi ya wakopaji.

Kijumla basi, hamna shaka kwamba mikopo ni namna ya kujiendeleza kiuchumi na ni sharti watu wakumbatie uwajibikaji mbele ya mikopo ili kujiepusha kujiingiza katika lindi la ufukara.

a) Tumia maneno 50 kuandika mawazo yanayodokezwa katika aya mbili za kwanza. (alama 5, 1 utiririko)
**Nakala chafu**
**Nakala safi**

b) Kwa kurejelea **aya za tatu hadi saba**, eleza hatari zinazowakumba wakopaji na **suluhisho** kwa hatari zenyewe. ( Maneno 75-85) (alama 8,1 utiririko)
**Nakala chafu**
**Nakala safi**

**3. <u>MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)</u>**

a) Andika **ufanano** mmoja kati ya sauti zifuatazo. (alama 2)
i) /v/ na /th/.......................................................................................................
ii) /t/ na /l/.......................................................................................................
iii) /k/ na /f/.......................................................................................................
iv) /m/ na /z/.......................................................................................................

b) Andika maneno yenye **miundo** ifuatayo. (alama 2)
i) Konsonanti, konsonanti, irabu, irabu.
ii) Konsonanti, irabu, konsonanti, konsonanti, irabu.

c) Andika neno lenye **mofimu** zifuatazo: (alama 2)
Kikanushi cha nafsi ya kwanza umoja, hali timilifu, yambwa, mzizi na kiishio.

d) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya **wingi**. (alama 1)
Wembe alionunua kwenye duka umemsaidia kukata ukucha.

e) Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya **ukubwa.** (alama 1)
Ng'ombe hawa na wale walivuka mto huo kwa utaratibu.

f) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo. (alama 3)
i) Mwanafunzi **<u>aliadhibiwa</u>** kwa kuwa **<u>alikosea</u>** mwalimu.
(Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino)
ii) Nguo zilinunuliwa juzi. Nguo ziliuzwa kwa bei ghali.
access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
(Unganisha kuunda **sentensi changamano**)
iii) Mapambano baina ya mwanadamu na mazingira yalizua fasihi. (Anza kwa: **Fasihi...)**

g) Tunga sentensi yenye **kishazi tegemezi** ambacho ni; (alama 3)
i) kivumishi
ii) kiunganishi
iii) cha masharti

h) Tunga senstensi moja yenye nomino katika ngeli ya U-I na kivumishi cha idadi. (alama 1)

i) **Ainisha** maneno katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Sahani tano safi zitatumika katika sherehe.

j) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika **hali ya mazoea**. (alama 1)
Kisu kinachonolewa ndicho kinachopata.

k) Eleza matumizi ya **'kwa'** katika senstensi ifuatayo. (alama 3)
Moja kwa tano ya watu waliosafiri kwa gari la moshi walikula wali kwa mchuzi.

l) **Akifisha** sentensi ifuatayo. (alama 3)
kahindi alipanda matatu nambari saba kisha akamuuliza dereva gari hili litanifikisha ukunda.

m) Kwa kutumia kitenzi kilicho katika mabano geuza sentensi iwe katika kauli uliyopewa. (alama 1)
Mgonjwa huyu hawezi ................ ....chakula mpaka apate fahamu. (pa-tendeka)

n) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)
KN (N + RH) + KT (t + E)

o) Nyooka ni kwa pinda,______________ni kwa dhahiri, na _____________ ni kwa hakika. (alama 2)

p) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya **kasi** na **kazi.** (alama 2)

q) **Kanusha** sentensi ifuatayo. (alama 2)
Viongozi wetu wazindukapo tutaacha kudhulumiwa na mataifa ya kimagharibi.

r) Ainisha **yambwa** katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Mwalimu aliwanunulia zawadi nzuri kwa shilingi elfu kumi.

s) Onyesha kwa kutumia sentensi mbili jinsi neno **shuleni** linaweza kuwa nomino na kielezi. (alama 2)

t) **Yakinisha** katika umoja. (alama 1)
Msipokuwa wenye bidii hamtayapata mafanikio maishani.

**4. <u>ISIMUJAMII (alama 10)</u>**
***<u>Soma kifungu kifuatacho halafu ujibu maswali.</u>***
"Baada ya mjadala mrefu kuhusu mswada huu na kuzingatia sheria za bunge hili tukufu, kifungu cha 4, kipengele cha 6, ibara ya 3, ndugu zangu ningependa kutangaza kupitishwa kwa mswada huu na sasa utawasilishwa kwa rais kusubiri sahihi yake. Kupitishwa kwa mswada huu kwa kauli moja ni tukio la kihistoria kwa bunge hili. Tutaweza kufikia the two third rule..."

a) Sifa mbalimbali za sajili ya bunge zinadhihirika katika kifungu hiki. Andika sifa zozote tano huku ukitoa mifano mwafaka. (alama 5)

b) Fafanua vipengele vingine vitano vya mitindo ya mawasiliano ambayo mbunge angetumia katika kufanikisha mawasiliano yake. (alama 5)

**KIGUMO CLUSTER**
**CHETI CHA KUFUZU MASOMO YA SEKONDARI**
**102/3**
**KISWAHILI KARATASI YA 3**
**FASIHI**
## SEHEMU A : USHAIRI

**1. Lazima** access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**Afrika**

Bara uliyetukuka na kusifika,
Unayevumbika asili yetu,
    Bara uliyekumbwa na vimbunga,
Vimbunga vya kila aina,

Tangu zama za utumwa hadi za leo, Bara
    usiyekata tamaa,

    Bara usiyejua kukimwa, Bara
    usiyejua kinyongo.

Ardhi yako imejaa hazina kochokocho, Batini
yako imefunika nemsi na utajiri,

    Unagombaniwa,

    Unapong'ang'aniwa,

Utajiri unaokugeuza kinyang'anyiro,
Kinyang'anyiro cha kushindaniwa.

Uso wako umeenea machozi tele, Machozi ya kilio cha
wanao, Wanaopigana vita kila uchao bila kujua kwani,

Kilio cha wanao wanaokufa njaa penye wingi wa mali, Kilio cha
waliao wakitamani kuiona haki, usawa na ukweli,

Wengine wanakukatia tamaa, sikati,
Wengine wanakulaani, silaani, Wengine
hawana matumaini, ninayo.

Najua iko siku,

Utasimama kama mlima kwa kujishasha,
Utanguruma kama simba mwenye kutisha, Siku
hiyo watajua Afrika bado haijawa.

(a) Eleza dhamira ya shairi hili. (alama 2)
(b) "Shairi hili ni la kutamausha." Thibitisha kwa mifano **tano** (alama 5)
( c) Fafanua umuhimu wa aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
(d) Eleza mitindo inayojitokeza katika shairi hili. (alama 4)
(e) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 1)
(f) Andika ubeti wa pili katika lugha nathari (alama 4)
(g) Eleza toni la shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU B: RIWAYA

**Assumpta K. Matei**: *Chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au*

2. (a) "Tathmini nafasi ya wimbo wa Shamsi katika kuijenga riwaya ya "Chozi la Heri." (alama 10)
(b) "Nilitaka kuhizika kwa kutamani kufa lakini nikauambia moyo wangu kwamba nimekufa japo sijafa." Kwa kurejelea hoja **kumi** kutoka kwenye riwaya hii, thibitisha kwamba mzungumzaji wa maneno haya anastahili kutamani kufa. (alama 10)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

3. "Niliichukia jaala iliyonipa mama anayejali masilahi yake tu, <u>nilichukia nguvu ya maumbile iliyoniweka kwenye jinsia ya kike</u> ..."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Andika toni ya kauli hii. (alama 2)
(c) Kwa kurejelea maisha ya mzungumzaji, bainisha vichocheo **sita** vya kauli iliyopigiwa mstari. (alama 6)
(d) Fafanua umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya katika kuijenga riwaya hii. (alama 8)

***SEHEMU YA C:HADITHIFUPI***

***TUMBO LISILOSHIBA NA HADITH INYINGINE(ALIFACHOKOCHO NA DUMU KAYANDA)***

***Jibu swali la 4 au 5***

***TUMBO LISILOSHIBA (S.AMOHAMMED)***

4 (i)` Hakuna aliyeweza kukitegua kitendawili chenyewe lakini…'
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama4)
b) Tambua mitindo uliyotumiwa katika dondoo hili. (alama2)
c) Fafanua chanzo na hatima ya kitendawili kinachorejelewa katika dondoo hili. (alama 6)
d) Eleza wasifu wa warejelewa katika dondoo hili. (alama4)
(ii) Huku ukirejerea hadithi ya Tulipokutana tena eleza namna unyanyashaji umeshughulikiwa (alama 4)

5. (a) Bainisha masharti ya kisasa yanayoongoza ndoa ya kisasa kwa mujibu wa hadithi ya "Masharti ya Kisasa." (alama 10)
(b) Kwa kurejelea "Shibe Inatumaliza", bainisha mchango wa raia katika kuizorotesha jamii yao. (alama 10)

**SEHEMU D: TAMTHILIA**
**Pauline Kea**: *Kigogo*

*Jibu swali la 6 au 7*

6. "Na hii Runinga ya Mzalendo nayo haina maisha Sagamoyo. Kitabakia kituo kimoja tu!"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Fafanua umuhimu wa anayeambiwa maneno haya. (alama 4)
   (c) Kando na kizingiti kinachojitokeza katika dondoo hili, bainisha vizingiti vingine **kumi na viwili** walivyokumbana navyo Wanasagamoyo katika kupambana na udhalimu jimboni. (alama 12)

7. "Ukitaka kuwafurusha ndege,katamti"
   (a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama4)
   (b) Onyesha mbinu nyingine zinazotumiwa na wahusika hawa kutimiza malengo yao. *(alama16)*

SEHEMU E: **FASIHI SIMULIZI**
8.
(a) *Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali.*
   Zamani, jamii mbalimbali ziliwasiliana kwa njia ya ngoma kutangaza kifo, kusherehekea mavuno mazuri na kadhalika.
   (i) Fasihi hii ya kuwasiliana na ngoma inaitwaje? (alama 1)
   (ii) Fasihi hii ilikuwa na dhima gani katika jamii? (alama 4)
(b) Bainisha majukumu **matano** ya nyimbo katika maigizo. (alama 5)
(c) Umepewa jukumu la kukusanya data ukitumia hojaji.
   (i) Eleza manufaa **matano** ya kutumia mbinu hii. (alama 5)
   (ii) Eleza changamoto **tano** za kutumia mbinu hii. (alama 5)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA KUTATHMINI WA JIMBO KIANGLIKANA LA NAMBALE 102/2**
**KIDATO CHA NNE**
**KISWAHILI KARATASI YA 2**

**JARIBIO LA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2021**

**1. UFAHAMU ( Alama 15)**

*soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

"Yakobo, eti babu yako ndiye mnyama? Siamini na sitaamini maneno hayo."

"Uliuomba ukweli."

"Kwa nini hukuniambia mambo haya zamani, Yakobo? Kwa nini mama yako hakunifunulia? Kwa nini aliisoma barua hii akaificha?"

"Yote hayo yalifanywa ili uwe na maisha bora. Ulipata wazazi wema waliokulea na kukutunza. Ulipelekwa shuleni, Chaanasa, mimi sikukanyaga shuleni. Ikiwa ungeachwa kinyongo, huenda hungekuwa na maendeleo uliyo nayo. Labda ungeingilia maisha mabaya na kuwa mtu bure kabisa. Zipo siri zinazowekwa ili kuwalinda watu."

Lakini, Yakobo, inaniuma sana. Miaka yote hii tumetembea pamoja, tumekuwa tukitembeleana, tumekula meza moja, tumefanya mambo mengi pamoja wala huniambii mimi ni mjomba wako."

Naomba msamaha, kwa moyo wangu wote, kwa kukosa kueleza mambo hayo mapema. Hata hivyo, ni vizuri kuona mambo kwa njia nyingi, si mtazamo mmoja tu. Tuseme, ningekuambia mambo hayo mapema, je, ungekuwa na furaha zaidi? Huenda jitihada zako za kumtafuta baba yako zingekutia chuki. Pengine hata ungetamani kulipiza kisasi kwa dhiki alizokuletea ukafungwa jela au hata kuhukumiwa kifo. Wakati mwingine, ni salama kutojua. Jambo usilolijua halikunyimi usingizi. Hata hivyo, naomba radhi kwa kutokuambia. Ukweli wa mambo ni kwamba hata Mzee Johari muungwana, yaani, babu yangu, au baba yako, hakujua mambo haya yote. Alikufa bila kujua sura au jina la mtoto wake: Chaanasa."

Bwana Chaanasa, bila kujua, alilia na kudondokwa na machozi kupukupu. Nikaona aibu kubaki hapo, lakini sikuondoka. Nilitaka kusikia hatima ya mazungumzo hayo.

"Yakobo, mpwa wangu," Bwana Chaanasa aliita huku akilia. Akanyoosha mikono yake na kumkumbatia Yakobo.

"Nimekusamehe. Nimekusamehe. Lazima nitekeleze ombi la mamangu. Alinisihi nisiwe na chuki na mtu yeyote. Siwezi kukuchukia mpwa wangu. Naahidi sitakuchukia kamwe. Asante kwa kuniambia ukweli wote. Asante pia kwa hekima yako kwani pia ulingoja hadi wakati unaofaa kunifunulia mambo haya. Ungaliyafunua zamani, kama ulivyosema awali, huenda nisingaliitikia jinsi nilivyofanya leo. Huenda mambo yangekuwa mabaya. Labda ningelipuka kwa hasira na kusababisha hasara, pengine hasara isiyolipika. Sasa ninaelewa kwa nini tunalandana sana nawe, na mzee Busara. Sisi ni wa damu moja. Baba yangu angalikuwa hai, ningalienda nikamwone na kujitambulisha kwake. Ningalimwita 'baba' na huenda angaliniita 'mwanangu.' Ningalimsamehe kwa kumwacha mamangu na kunitelekeza."

"Bado unaweza kumsamehe."

"Jinsi gani?" Bwana Chaanasa akauliza.

"Kwa kusahau yaliyopita na kuganga yajayo. Yazike mambo yote hayo katika kaburi la sahau. Acha ya kale yawe ya kale, ya nyuma yawe ya nyuma, ya zamani yawe ya zamani. Kilichotendeka kimekwishatendeka. Yaliyofanyika yamefanyika. Yamemwagika na hayatazoleka kamwe hata kwa kuchimbua ardhi. Lililopita limepita, si uwele tena.

"Naam, Bwana Chaanasa, lipitalo hupishwa."

(a) Eleza sababu za Chaanasa kufichwa taarifa kuhusu babake. (Alama 2)
(b) Thibitisha kuwa babu yake Yakobo alikuwa mnyama. (Alama 2)
(c) Eleza umuhimu wa maswali balagha katika kifungu hiki. (Alama 2)
(d) Je, ni kweli kuwa kama si kuweka siri mambo yangemharibikia Chaanasa? Tetea jibu lako. (Alama 3)
(e) Ni jambo lipi lililomfanya Chaanasa kumsamehe mpwa wake? (Alama 2)
(f) Kwa mujibu wa kifungu, kusamehe kuna matokeo gani? (Alama 2)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. (Alama2)
access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
(i) hayatazoleka
(ii) tunalandana

## 2. UFUPISHO ( Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Maadili ni desturi, utamaduni au hulkaa mbazo hubainisha na kulipa kundi fulani la watu upekee wake. Maadili ni muhimu katika kuonesha imani na kanuni za maisha ambazo kundi Fulani la watu huchukulia kuwa chanya na zile wanazozichukulia kuwa hasi. Maadili ndio mwongozo unaothibiti matendo na hulka za kila mmoja.

Kila jamii huwa na maadili yake ambayo yanamhitaji kila mwanajamii kutenda na kuishi kama jamii inavyotarajia. Pia, yaliweza kulegeza mielekeo au mitazamo yao. Hata leo, maadili hutusaidia kubainisha sisini akina nani, mtazamo wetu maishani, pamojana matarajio yetu.

Katika Katiba ya Kenya, maadili ya jamii ya Wakenyayameangaziwavyema. Kwanza, ni wazi kuwa Kenya ni taifa la wacha Mungu, kwa hivyo, kila Mkenyaanatarajiwa kuabudu na kumheshimu Mwenyezi Mungu. Hili limeshadidiwa hata katika wimbo wetu wa taifa. Pamola na hayo, katika kuimarisha umoja wa kitaifa, tofauti zetuWakenya kirangi, kikabila, kitabakana hata kidini hazipaswi kutugawanya.Maadili yanatuhimiza kuzichukulia hizo kuwa sifa za kipekee na kuzionea fahari. Ule utaifa wetu kama wakenya unapaswa kuwekwa mbele daima ili kuzima juhudi zozote za kututenganisha kwa misingi hiyo.

Kama taifa, tunahitaji kudumisha uzalendo wetu kwa kujitolea kuhakikisha kuwa mahasidi hawaporomoshi maadili ya jamii zetukwa kuiga hulka zao potovu. Uzalendo unatuhumiza kuripoti vitendo vyote vya kuihujumu nci au watu wake kwa asasi za dola. Asasi hizo zitachunguza na kuzima utekelezaji wa uhalifu kabla haujatikea, na iwapo utakuwa umetokea, asasi hizo zitawapa adhabu wahalifu ili waweze kubadili mienendo mibaya na kuwa kielelezo kwa wengine wenye nia mbaya.

Maadili, vilevile, humwongoza mtu kuhusu namna za kutatua mizozo na kudumisha amani. Hatuwezi tukajivunia uhuru pasi na kuwepo amani. Amani ndio msingi wa umoja, ustawi na maendeleo ya taifa lolote. Ukosefu wa amani hudumaza na hata kurudisha nyuma maendeleo kwa kuwahini watu nafasi za kushiriki uzalishaji mali. Ukosefu wa amani vilevile husababisha kuongezeka kwa visa vya uhalifu kama vile mauaji,

kulememazwa kwa watu, unajisi, uharibifu wa mali na kusambaratika kwa familia, hali ambayo huchangia mporomoko wa maadili katika jamii.

Uadilifu unakwenda kinyume na methali, amani haiji ila kwa ncha ya upanga. Ukweli ni kwamba, tunaweza kusuluhisha tofauti zetu bila kutumia silaha. Matumizi ya silaha aghalabu huzidisha uhasama na kuchochea haja ya kulipiza kisasi. Njia pekee ya kutatua migogoro ni kuelewa chanzo cha migogoro yenyewe, wahusika kufanya kikao na kuizungumzia kwa uwazi na kwa utulivu. Pande zote husika zinafaa kukubali makosa au madhara yaliyotokana na matendo yao na kuomba msamaha ili kupata maridhiano. Kuomba msamaha kusidhaniwe kuwa kujishusha hadhi, bali ni unyenyekevu katika kutatua tofauti kwa manufaa ya muamala wa vizazi vijavyo. Anayeombwa msamaha naye anapaswa kuwa tayari kutoa shifaa kwa dhati na kusahau kosa alilofanyiwa. Yote haya yakishindikana, mgogoro wapaswa kupelekwa mahakamani. Haki za kila mmoja zimelindwa katika katiba yetu na mahakama zipo ili kutetea haki hizi bila kupendelea upande wowote.

Utiifu wa sheria vilevile ni njia mojawapo ya kukuza maadili ya kijamii. Kwa kuwa sheria hulinda haki za kila mtu; wake kwa waume, wakubwa kwa wadogo, kila mmoja ana wajibu wa kuheshimu sheria. Hii ni pamoja na kulinda rasilimali zetu kama jambo la wajibu bila ya kutegemea kuwepe wadumisha sheria. Uongozi wa kisheria huwapa watu hakikisho kuwa maisha yao hayatakuwa kama ya mahayawani nyikani bali yatafuata utaratibu Fulani. Hivyo basi, sheria ni hakikisho la jamii inayolinda haki na kuendesha mambo yake kwa uwazi, haki na ushwari.

Bila shaka, tukizingatia na kuimarisha maadili, taifa letu litakuwa jamii bora na kivutio cha kila mtu. Kiu ya Wakenya ya kutaka kuhamia nchi nyingine, hasa zilizostawi, itapungua. Wote watakuwa na ari ya kuliendeleza taifa lao.

MASWALI

a) Eleza umuhimu wa maadili kwa jamii na taifa kwa ujumla. (maneno 60-70) ( alama 7 , 1 ya utiririko)
Nakala ya matayarisho
Nakala safi

b) Fafanua jinsi mizozo inaweza kutatuliwa kwa uadilifu. (Maneno 75-80) (alama 8, 1 ya utiririko)
Nakala ya matayarisho
Nakala safi

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**3. MATUMIZI YA LUGHA ( Alama 40)**

(a) (i) Kwa kutoa mfano mwafaka, fafanua dhana ya kiambishi. (Alama 2)
(ii) Eleza dhima ya viambishi katika neno lifuatalo. (Alama 3)
lililolilia

(b) Andika neno lenye muundo wa IKKKI. (Alama 1)

(c) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo.
i) Mwanagenzi mwenyewe aliimba wimbo vizuri. (Alama 1)
ii) Vyakula vyetu vina ladha nzuri sana. (Alama 2

(d) Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo: (Alama 2)
i) Kikwamizo cha meno hafifu
ii) Kikwamizo cha kaa kaa gumu
iii) Irabu ya chini kati
iv) Nazali ya kaa kaa laini

(e) Andika sentensi ifuatayo katika hali tegemezi. (Alama 1)
Watakapokuwa wakicheza kandanda tutakuwa tumelala fo fo fo.

(f) Onyesha ngeli za maneno haya. (Alama 2)
i) nyavu
ii) wizani
iii) miadi
iv) mwalishi

(g) Mbali na kuorodhesha, onyesha matumizi mengine mawili ya koloni. (Alama 2)

(h) Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi. (Alama 2)
Wapishi wameandika meza haraka ipasavyo.

(i) Andika sentensi moja ili kuonyesha maana mbili za neno **ila.** **(**Alama 2)

(j) Andika sentensi ukitumia vitenzi vitokanavyo na nomino zifuatazo. (Alama 2)
i) hofu
ii) somo

(k) Andika sentensi yenye kishazi tegemezi vumishi cha wakati ujao. (Alama 2)

(l) Pigia mstari kihusishi na uonyeshe kinaashiria nini? (Alama 2)
 (i) Mwalimu amesimama karibu na mlango.
 (ii) Mzee anapoketi huona mbali kuliko kijana anaposimama.

(m) Changanua sentensi ifuatayo kwa mtindo wa matawi. (Alama 3)
Mbuzi na kuku walikuwa wakiuzwa sokoni.

(n) Badilisha katika kauli ya ketendua. (Alama 2)
Tulitundika picha hiyo na kuyabandika maandishi ukutani.

(o) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hii. (Alama 2)
Yeyote atakayefika katika mkutano wa chifu atakaribishwa vizuri.

(p) Andika katika usemi wa taarifa. (Alama 2)
"Ziara ya Rais wetu itakamilika kesho alasiri." Msemaji wa ikulu alimwambia mtangazaji.

(q) Andika sentensi moja ukitumia kihisishi cha kuridhia. (Alama 1)

(r) Onyesha tofauti za kimaana za neno **zuka** na **suka** katika sentensi moja. (Alama 2)

(s) Geuza katika ukubwa. (Alama 2)
Ng'ombe walivunjika miguu yao

(t) Tunasema kishazi cha samaki , ________________ wa samaki au ____________________ ya samaki (Alama 1)

**4. ISIMUJAMII (Alama 10)**
(a) Kwa kutoa mifano mwafaka eleza visababishi vitano vya kuchanganya ndimi. (Alama 5)
(b) Kiswahili ni **lingua franka.** Thibitisha kwa mifano madhubuti. (Alama 5)

**MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA KIANGLIKANA 2021**
**DAYOSISI YA NAMBALE**
**MUHULA WA PILI**
**KIDATO CHA NNE – KISWAHILI KARATASI YA 3**

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU A: HADITHI FUPI**
**SHIBE INATUMALIZA NA SALMA OMAR HAMAD**

1. **SWALI LA LAZIMA**
"… Na ati tuliopewa hatupokonyeki…"
a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (al 4)
b) Taja mbinu **mbili** za sanaa zilizotumika katika dondoo hili (al 4)
c) Fafanua sifa zozote **nne** za mzungumzaji (al 2)
d) Kwa kurejelea hadithi 'shibe inatumaliza' tathmini jinsi ubadhirifu wa mali ya umma umesawiriwa katika hadithi hii (al 10)

**SEHEMU YA B**
**RIWAYA: CHOZI LA HERI: ASSUMPTA MATEI**

2. "…liandikwalo ndilo liwalo? since when has man ever changed his destiny?"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
b) Bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (al 6)
c) Kwa kuzingatia hoja **kumi**, jadili jinsi ambavyo hali ya, **liandikwalo ndilo liwalo",** inavyojitokeza katika Chozi la Heri. (al 10)

Au

3. Maovu yametamalaki katika riwaya ya **Chozi la Heri.** Thibitisha (al 20)

**SEHEMU C**
**TAMTHILIA: KIGOGO**

***4.*** "na uuchunge sana ulimi wako usikutome kwenye bahari mchafukoge usi…"
a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (al 4)
b) Eleza sifa **mbili** za msemaji (al 2)

c) Eleza umuhimu wa msemewa katika kazi hii (al 2)

d) Kwa kurejelea dondoo hili na tamthilia kwa jumla, eleza jinsi msemewa na wenzake walitiwa katika bahari mchafukoge. (al 12)

**AU**

***5.*** Tamthilia ya Kigogo ni ya kisasa. Thibitisha ukweli wa kauli hii. (al 20)

***6.*** **SEHEMU YA D: USHAIRI**

***Jibu swali la sita au la saba***

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Msambe naja kuteta, nina wema wa kalima,
Moto wanikatakata, maini yangu yachoma,
Ili nipate takata, ukweli wote 'tasema,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Bahati ni kama nyota, humemeta na
Kuzima, Sikimbilie mafuta, ukatae
Kula sima, Anayekataa pema,
pabaya Panamuita.

Haraka zina matata, angaza mbele na
Nyuma, Tenda mambo kwa kusita,
Usije ukalalama, Keti pako ukipata,
Kwa muradi wa uzima, Anayekataa
Pema, pabaya panamuita.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Pema si penye mafuta, au pa wali
Na nyama, Pema watu hutafuta,
Utulivu na hekima, Si hoja penye
Ukata, pa watu hali ya nyuma,
Anayekataa pema, pabaya
Panamuita

Mahali pema ambata, kwa vitendo na huduma,
Sikae penye matata, palipojaa hasma,
Lau kama pamemeta, hapafai kwa daima,
Anayekataa pema, pabaya
panamuita

**Maswali**

a) Lipe anwani mwafaka shairi hili. (alama 1)

b) Bainisha bahari mbili za shairi hili. (alama 2)

c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

d) Fafanua dhamira ya mshairi. (alama 1)

e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

f) Onyesha jinsi mshairi alivyotumia uhuru wake. (alama 3)

g) Kwa kutoa mifano, bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)

h) Eleza maana ya msamiati ufuatao. (alama 3)

i) Kalima I i) Mafuta iii) Ukata

7. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

1. Mbiu naipuliza, kwawa hapana ng'ambo,
Kwa aningoja 'mesikia, inaumiza matumbo,
Kwa upole sitafyoa, hata kamna kwa kimombo, Yafaa
jihadharia, maisha ya s'ende kombo.

2. Maisha ya s'ende kombo, kututoa yetu ari,
Zingatia haya mambo, wetu wale zimukiri, Kuwa
wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri
watunzeni na maumbo, msie zusha hatari.

3. Msije zusha hatari, na nyingi hizi zahama,
Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama
Twaelezea kwa uzuri, matendoyo yatuuma Watoto
tunayo mori, ni lini mtaja koma?

4. Ni lini mtaja koma, na pombe siso halali?
Sio baba sio mama, mbona ny' hamtajali? Mwafa ja
nzi twasema, mwatua chabi la hali Hangaiko acha
nyuma, kwani hamuoni hili?

5. Kwani hamuoni hili, kila saa mwapigana Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona Mwatusumbua akili,
twaumia ten asana Achene na ukatili, kwani upendo hamna.

6. Kwani upendo hamna, kamam mbwa mwatuchapa
Mwatuchoma sisi wana, mio yetu yatupapa
Pa kujificha hatuna, tumebaki tukitapa

7. Tumevujwa na mifupa, hata leo uke wetu, access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
Mwatubaka na kuapa, kutung'ata nyi' majitu,
Hayo makeke na pupa, mtakoma utukufu

8. Mtakoma utukufu, nakutumia miki
Na tabia zenye kutu, tumechoka nayo chuki
Hatutakubali katu, kutendewa yenye siki Serikali
fanya kitu, kwani nasi tuna haki

**Maswali**

a) Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
b) Taja nafsi nne katika shairi hili. (alama 1)
c) Eleza bahari mbili zinaowakilishwa katika shairi hili. (alama 4)
d) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)
e) Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)
f) Eleza umuhimu wa mbinu mbili amabazo mshairi ammetumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8. Hamkuona jinsi tulivyowapiga magoli
   Hamkuona vile tuliwala chenga kila mara
   Itakuwaje timu mbovu kama hii
   Kuchezea miamba kama sisi
   Niliwafunga baada ya sekunde wakati ule nitashindwaje leo?

**Maswali**

(a) Tambua kipera kinachodokezwa na maelezo haya na ukifafanue (al 2)
(b) Fafanua umuhimu wa kipera cha fasihi ulichotambua katika (a) (al 8)
(c) Fafanua sifa zozote tano za mawaidha (al 5)
(d) Ni changamoto zipi zinazoweza kumkumba mtafiti akifanya utafiti wa soga nyanjani (al 5)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

–

–
–
–
–

–
–
–

**LANG'TA/KIBRA**
**102/1**
**KISWAHILI**
**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2021**
**INSHA**

1. Wewe ni Mkurugenzi wa tume ya kupambana na ufisadi nchini. Andika barua pepe kwa watumishi wote wa umma ukiwaeleza athari za ufisadi kwa taifa.

2. Teknolojia ya kisasa ina athari mbaya katika maisha ya vijana. Jadili.

3. Andika insha itakayodhirisha maana ya methali ifuatayo: Mzaha mzaha hutumbuka usaha.

4. Andika kisa kitakachomalizika kwa … hivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha Yangu ulivyofunguka.

**LANG'ATA/KIBRA**
**102/2**
**KISWAHILI Karatasi ya 2**
**MUHULA WA PILI 2021 KIDATO CHA NNE**

**1. UFAHAMU: (Alama 15)**

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia</u>**

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanaoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizotukuka zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hili husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto, awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hili walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. <u>Inakera</u> zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa Jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea had kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa, ni kweli. Hata hivyo, wengi hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21, asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa <u>majukumu</u> mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyishwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo nakuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata awaoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale hushia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine hushia kutumiwa kama watumwa wa 'kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali 'mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

**Maswali**

**a)** Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 1)**

**b)** Eleza dhana ya mwanamkiwa kwa mujibu wa kifungu. **(alama 2)**

**c)** Eleza imani za kijadi kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 2)**

**d)** Jadili masaibu yanayowakumba wanawakiwa. **(alama 4)**

**e)** Eleza haki mbili za kikatiba zilizokiukwa kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 4)**

**f)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu. **(alama 2)**

- **i)** Inakera
- **ii)** Majukumu

**2. UFUPISHO: (Alama 15)**

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali</u>**

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundishia. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkemu kwa mtu wa kila rika. Halikadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji wa stadi ya kujifundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemchemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanaowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii. Ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaotumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

a) Fupisha aya tatu za kwanza za (maneno 70 – 75) (alama 7, 2 za utiririko)
Matayarisho
Jibu

b) Eleza udhaifu wa runinga na video. (maneno 50 – 51) (alama 5, 1 ya utiririko)
Matayarisho

**3. MATUMIZI YA LUGHA:** **(alama 40)**

**a)** Taja aina mbili kuu za ala za kutamkia sauti **(alama 2)**

**b)** Taja mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo **(alama 2)**
Kimadende____________________________________________________________
Kipasuo kwamizo________________________________________________________

**c)** Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi sahili **(alama 2)**

**d)** Ainisha mofimu katika neno lifuatalo **(alama 3)**
Tulimpikia_____________________________________________________________

**e)** Ainisha vitenzi katika sentensi: Kitabu anachotaka kusoma ki mezani **(alama 3)**

**f)** Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi kiteuzi **(alama 2)**

**g)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama 2)**
a) Uzi____________________________
b) Muda___________________________

**h)** Tumia ‘o’ rejeshi ya kati katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Watu ambao walifika jana ni wale ambao walitoka mbali

**i)** Onyesha shamirisho kipozi na ala katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Mwindaji haramu alimuua ndovu kwa bunduki

**j)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 3)**
Kilipikwa jana jioni

**k)** Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi **(alama 2)**
Msingesoma kwa bidii, msingepita

**l)** Tunga sentensi moja kudhihirisha dhamira/jukumu hili **(alama 2)**
Rai/ombi

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**m)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Mtoto ambaye alianguka jana ana maumivu mengi

**n)** Onyesha matumizi yoyote mawili ya kiwakifishi: koma/kituo_ _ _ _ _ . **(alama 2)**

**o)** Tumia neno ‘Nairobi’ kama **(alama 2)**
**a)** Nomino
**b)** Kielezi

**p)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya kuku na gugu **(alama 2)**

**q)** Onyesha matumizi ya kiambishi -ji- katika sentensi **(alama 2)**
Mwongeleaji stadi anajishaua sana.

**r)** Andika katika usemi wa taarifa **(alama 2)**
“Wageni wangu watafika saa ngapi? Mama aliuliza

**s)** Unda nomino kutokana na kitenzi **(alama 1)**
Safari

**4. ISIMUJAMII:** **(alama 10)**
Nipe chai, andazi mbili na egg moja………….
a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya **(alama 2)**
b) Fafanua sifa nne zinazohusishwa na sajili hiyo **(alama 8)**

**LANG'ATA/KIBRA**
**102/3**
**KISWAHILI KARATASI 3 (FASIHI)**
**DECEMBER 2021**

**SEHEMU YA A: TAMTHILIA**
**P.Kea:Kigogo**
***1. Lazima***
(a) Jadili jinsi kumi ambazo maudhui ya ukatili yanajitokeza katika Tamthilia ya Kigogo (alama 10)
(b) Eleza mifano kumi ya matumizi ya kinaya katika Tamthilia ya Kigogo. (alama 10)

**SEHEMU YA B**
**RIWAYA: CHOZI LA HERI**
*(Assumpta K. Matei)*
Jibu swali la Pili au la Tatu
2. "Watu husema kuwa binadamu hawawi sawa ila kifoni…"
a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alalama 4)
b) Tambua mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
c) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya. (alama 6)
d) Thibitisha kuwa hakuna usawa baina ya wanadamu. (alama 8)
**Au**
3. Jadili nafasi ya sehemu zifuatazo katika riwaya ya Chozi la Hari:
(a) Hotuba (alama 10)
(b) Uozo katika jamii (alama 10)

**SEHEMU C**
**HADITHI FUPI**
(Mtihani wa maisha)
'Leo mwalimu mkuu atajua kwamba mdharao biu hubiuka'
(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)
access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
(b) Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika mktadha huu. (Alama 6)
(c) Eleza wasifu wa mzungumzaji wa maneno haya. (Alama 2)
(d) Jadili maudhui ya elimu kama yanavyojitokeza katika hadithi hii. (Alama 8)
(Ndoto ya mashaka (Ali Abdulla)

**(5)** 'Kusema kweli lakini hata mimi sikuwa na nadhari katika kumpenda msichana huyu … Nilimpenda kufa! Lakini! Kwao bure tu!'
(a) Eleza mkutadha huu. (Alama 4)
(b) Taja mtindo wa lugha uliotumika katika mkutadha huu. Alama 4
(c) Taja sifa mbili za mzungumzaji. (Alama 2)
(d) Onyesha maudhui ya umaskini katika hadithi fupi ya Ndoto ya mashaka.

**SEHEMU YA D**
***USHAIRI***
*Jibu swali 6 au 7*

(6) **USHAIRI**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**
Daima alfajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu;
Ni miti yote hujipinda migongo
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua

Akichekelea ha ha ha ha ha ha ha …
Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho;
Kuna jambo gani linamridhisha?
Kama si kujua ni kutokujua
Laiti angalijua, laiti angalijua!

(a) Eleza matatizo manne yanayompata mzungumziwa. (Alama 4)
(b) Eleza mtindo wa lugha uliotumiwa na mshairi na utoe mifano. (Alama 8)
(c) Taja nafsineni katika shairi hili. (Alama 1)
(d) Eleza toni ya shairi hili. (Alama 1 )
access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
(e) Taja mbinu mbili za uhuru wa kishairi uliotumika na utoe mifano. ( Alama 2)
(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

**(7) Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili

Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ila ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili.

Vingekuwepop viraka, kuutia, ngeushuruti mwili
Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili
Upya ukaungilika, kuvutia, roho na wake mwili.

Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
Sihofu kupata mawi, sitajua, kupigania mwili
Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili.

Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika, damu, jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili.

(a) Liweke shairi hili katika bahari tatu. (Alama 3)
(b) Eleza dhamira ya mshairi. (Alama 2)
(c) Eleza muundo wa shairi hili. (Alama 4)
(d) Toa mifano ya uhuru wa kishairi uliotumika. ( Alama 4)

(e) Eleza kwa kifupi maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (Alama 3)

(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (Alama 4)

**SEHEMU D**

**FASIHI SIMULIZI**

A (i) Miviga ni nini? (Alama 2)

(ii) Eleza sifa nane za miviga. (Alama 8)

B (i) Ulumbi ni nini? (Alama 2)

(ii) Eleza sifa nane za ulumbi (Alama 8)

–
–
–
–
–
–
–
–
–

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**3.**

–
–
–
–

**MTIHANI WA PAMOJA WA GATUZI NDOGO-BUTULA**
**KISWAHILI 102/1**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

**MASWALI**
**LAZIMA**

1. Wewe kama rais umekerwa na kukithiri kwa ufisadi katika wizara mbalimbali. Andikia memo mawaziri wako ukiwaeleza madhara ya ufisadi na hatua utakazochukua ikiwa hawatakomesha ufisadi katika wizara zao. (alama 20)
2. Visa vya utovu wa nidhamu miongoni mwa wanafunzi huongezeka katika muhula wa pili na wa tatu. Fafanua vyanzo na madhara ya hali hii. (alama 20)
3. Andika kisa kinachoafiki methali:….Ukicheza ujanani, utalipa uzeeni. (alama 20)
4. Andika insha itakayokamilika kwa maneno yafuatayo:
   …waliwasili saa tatu baadaye. Uharibifu wa mali na maisha ulikuwa umeshatendeka. Kufika kwao hakukusaidia kwa lolote. (alama 20)

**MTIHANI WA MWIGO WA GATUZI NDOGO LA BUTULA**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma. Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano, kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho na nyinginezo kwa raia, kuna hatari

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya.
Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini. Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikalikama vile magari, nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyikazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma kupeleka vituo vyao vya afya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umma wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, wahandisi, mawakili, walimu na mahasibu ambao hukwepa majukumu yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi. Wengine wasio wataalamu huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwingine hulazimika kusalimu amri na kutoa hongo hili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale wasiojimudu kifedha hubaki wakilia ngoa. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza kuhudumia jamii.

Ufisadi umekita mizizi na kushamiri katika sekta za umma za kibinafsi kwa upande wa kuajiri

wafanyakazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyakazi wasiohitimu na wasiowajibika kazini.
Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufisadi. Kwa hivyo, wafanyakazi wenye bidii hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimebuniwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza Kashfa ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia siziso halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo. Serikali pia imeunda kamati ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi waliohasiriwa na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa kuwalipa au kuwatetea mahakamani ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

**Maswali**

a) Eleza aina nne za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma. (alama 4)
b) Kulingana na kifungu ulichosoma,ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani ? (alama 2)
c) Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi ? (alama 3)
d) Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini ? (alama 2)
e) Toa msamiati mwingine wenye maana sawa na rushwa (alama 1)
f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kifunguni: (alama 3)
   i) shamiri ________________________________
   ii) waliohasiriwa ________________________________
   iii) wakilia ngoa ________________________________

**2. UFUPISHO ( ALAMA 15)**

*Soma Makala haya kisha ujibu maswali.*

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**Umuhimu wa vyombo vya habari**

Vyombo vya habari hutumika kupasha watu habari kutoka upande mmoja hadi mwingine. Vyombo hivi vina manufaa kwetu. Vyombo hivyo ni kama vile runinga, redio, magazeti, tarakilishi na vinginevyo. Umuhimu mmoja wa vyombo hivi ni kueleimisha. Watu huelimishwa kuhusu jinsi ugomvi unaweza kuepukika katika familia. Pili huelimishwa juu ya magonjwa tofauti kama vile ukimwi, kipindupindu na mengine na jinsi ya kujikinga au kupata matibabu.

Mbali na hayo, vyombo hivi hutumika kuarifu. Watu huarifiwa kuhusu serikali yao, hususan jinsi mambo yanavyoendeshwa, uhusiano kati ya wajumbe serikalini na hapo kuwaacha watu na maarifa ya kufanya uamuzi bora utakaowanufaisha. Vyombo hivi pia huarifu kuhusu matukio kama ajali za barabarani, majumba kuchomeka na hata mashambulizi ya kigaidi pamoja na matukio mengine. Hiini muhimu kwani watu huwa na habari kuhusu yanayoendelea.

Vyombo hivi, kwa upande mwingine, huchangia kwa kiwango kikubwa umoja wa wananchi. Watu waishio sehemu mbalimbali wanaweza kufahamu vile wenzao katika sehemu nyingine waishivyo kutokana na lelemama, michezo ya kuigiza na kadhalika kutoka sehemu moja hadi nyingine. Chambilecho wahenga umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Fauka ya hayo, vyombo hivi ni muhimu kwani kupitia kwavyo watu wengi wameweza kupata gange. Watu hawa ni kama vile waandishi wa habari, wahandisi wa mitambo, watangazaji na kadhalika. Wao huweza kujimudu, kumudu familia zao na hata kukuza uchumi.

Vyombo vya habari ni muhimu kwa kuwa ni vyombo vya kutumbuiza vilvile. Kutokana na kutumbuizwa, waliotoka kufanya kazi za sulubu hata kazi zingine zozote huweza kupumzika vyema kwa kuburudishwa na hivyo kuwa wachangamfu tena. Mbali na kupumzisha wanaoandaa burudani kama vile muziki na maigizo kupitia kwa vyombo hivi vya habari hasa vijana huweza kupata hela za kujikimu na hivyo basi kujiepusha na visa vya uhalifu, mihadarati na hata uasherati.

Mwisho, vyombo vya habari hutumiwa na wanasiasa wakati wa uchaguzi ili kueneza manifesto zao na za vyama vyao. Kupitia kwa vyombo hivi, wananchi kote nchini wanaweza kujua kujua wanasiasa ambao wananuia kuleta maendeleo na hivyo kufanya maamuzi yao wakati wa uchaguzi.

Aidha, kupitia kwa vyombo hivi tume ya uchaguzi inaweza kuwaeleza wananchi kuhusu mambo ambayo wanafaa kujiepusha nayo, kwa mfano kupokea hongo ili kutovunja sheria za uchaguzi.
Kwa jumla vyombo vya habari ni muhimu katika maisha ya jamii. Vyombo hivi vinafaa kutumiwa ipasavyo ili navyo viwatumikie wananchi kwa njia mwafaka. Vyombo hivi vikitumiwa visivyo vinaweza kuleta hasara kubwa na hata maangamizi.

**MASWALI**

a) Kulingana na Makala, vyombo vya habari vina wajibu gani katika jamii? ( maneno 60)
Matayarisho
Jibu

b) Mbali na umuhimu wa vyombo vya habari, vyombo hivi vinaweza kuletea jamii hasara kwa njia nyingi. Eleza ( Maneno 50) ( Alama 7, moja mtiririko. )
Matayarisho
Jibu

**3. *<u>MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)</u>***

(a) Tambua na utolee sababu sauti ambazo hazifai kuwa miongoni mwa zile zilizotajwa hapo chini ( alama 2)
/ch/, /g/, /j/, /k/

(b) Bainisha mofimu katika utungo ufuatayo: ( alama 3)
Hakumjia

c) Kwa kutolea mifano, taja matumizi manne ya kiambishi m (al 2)

d) Eleza majukumu mawili ya sentensi ifuatayo. ( Al2)
Panda mtini na uangue matunda kwa vile yameiva vizuri.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

e) Tunga sentensi kwa kutumia kitenzi cha silabi moja chenye maana ya kuogopa katika kauli ya kutendeka. (alama 2)

f) Ainisha kielezi katika sentensi ifuatayo na ukibadilishe kiwe kiwe kielezi igizi (al 2)
Mbwa yule mweusi alibweka kwa hasira

g) Bainisha mwingiliano wa maneno katika sentensi hii (al 2)
Wanafunzi walifanya haraka japo haraka yao iliwatia taabani.

h) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari (al 1)
<u>Naam</u>... ameleta <u>machache.</u>

i) Tunga sentensi moja kwa kutumia kihisishi cha masikitiko (al 2)

j) Yakinisha katika udogo wingi (al 2)
Ng'ombe yuyu huyu hajazaa ndama mkubwa

k) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi mawili ya kibainishi (al 2)

l) Andika katika usemi halisi. (al 2)
Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo.

m) Maneno yafuatayo yamo katika ngeli zipi (al 2 )
wembe____________________________________________________________
mnyoo____________________________________________________________

n) Tambua kiima na yambwa katika sentensi ifuatayo (al 2)
Daktari yule hupigiwa nguo pasi na halima

o) Ainisha fungu la maneno lenye muundo wa kiima na kiarifa ambalo linakamilika au lisilokamilika kimaana katika sentensi ifuatayo (al 2)
Mtoto huyu atapita mtihani iwapo atasoma kwa bidii

p) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu (al 2)
Msomi hakutuzwa siku hiyo

q) Pambanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha vishale (al 4)
Letu lililopaliliwa limetuletea mazao mengi.

r) Amechanjiwa kuni ina maana ya kutenda kwa niaba ya.Eleza maana nyingine mbili zinazobainishwa na sentensi hii. ( Al 2)

s) Tia nanga ni fika na___________ ni kuwa na wivu (al 1)

t) Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo (al 1)
Kupanda mchongoma,kushuka ndio ngoma
Anza kwa Kushuka...........

**4. ISIUMUJAMII (ALAMA 10)**

a) Taja mambo manne yanayopelekea kufa kwa lugha (al 2)
b) Kwa mifano minne,elezea namna muktadha unavvyoathiri mitindo ya lugha (al 4)
c) Ukiwa mkaguzi mwakilishi katika mashindano ya kiswahili ,fafanua na kueleza mambo yanayochangia wanafunzi kufanya makosa ya kisarufi na ya kimatamshi katika lugha ya Kiswahili ( al 4)

**MTIHANI WA MUUNGANO WA SHULE ZA JIMBO NDOGO LA BUTULA**
**102/3**
**KISWAHILI KARATASI YA 3**
**FASIHI**

**SEHEMU A: USHAIRI**

**SWALI LA LAZIMA**

1. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyatubu
Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha wenye raha na tabu,ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina,Saidi Ali Rajabu
Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, Ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja wenye dini, wamtiio wahabu
Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu
Mapadiri kanisani, huvihubiri vitabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa na moyo kisebusebu
Tunakaribia kuja, kwa kushindwa kujimudu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
Na wengine sitotaja, msinambe ninagubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani ifaayo. (alama 1)
(b) kwa kutoa mfano, eleza mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (alama 2)
(c) Eleza jinsi uhuru wa mshairi ulivyotumika katika shairi. (alama 2)
(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (alama 4)
(e) Taja na ueleze bahari zozote mbili zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)
(f) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
(g) Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)
(h) Fafanua dhamira ya mshairi. (alama 2)
(i) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (alama2)
(i) Malofa:
(ii) Udubu:

**SEHEMU B: RIWAYA**
**CHOZI LA HERI**
**JIBU**

2. "Nyamaza wewe! Nyinnyi ndio mnaoturudisha nyuma miaka yote hii!"
(a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
(b) Kwa kurejelea hoja saba, eleza jinsi msemaji alivyorudishwa nyuma (alama 7)
(c) Eleza umuhimu wa msemaji katika riwaya (alama 6)
(d) Eleza toni ya dondoo hili (alama2)
(e) Toa sifa moja ya msemaji katika dondoo hili. (alama1)

**AU**

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

3. Jadili nafasi ya sehemu zifuatazo katika riwaya ya Chozi la Heri:
(a) Hotuba (alama 10)
(b) Uozo katika jamii (alama 10)

**SEHEMU C:TAMTHILIA**
**KIGOGO**
**JIBU**

4. " Sitaki kazi za uchafu hapa …"
(a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
(b) Kwa kurejelea hoja kumi, onyesha jinsi **kinaya** inajitokeza katika tamthiliya (alama 10)
(c ) Fafanua sifa sita za msemaji (alama 6)

**AU**

**5**. " Do!Do!Si mameni !Si mameni ! leo kutanyesha mawe!"
i) Eleza muktadha wa dondoo hili ( Alama 4)
ii) Fafanua mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili ( alama 4)
iii) Huku ukitoa mifano jadili hoja sita zinazodhihirisha jinsi mwanamke alivyasawiriwa katikaTamthilia ya Kigogo ( alama 12)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**
**TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**
**JIBU**
(Tulipokutana Tena)

**6**. "Mnaruka tu hewani kama ndege mkitumia uchawi wenu…
Nani kakuambia upuuzi huo?"
(a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
(b) Eleza mbinu moja katika dondoo hii (alama 2)

(c) Dondoa maudhui moja kutoka kwa dondoo hii (alama 2)
(d) Jadili matatizo nane yanayomkumba mhusika Bogoa (alama 8)
(e) Fafanua umuhimu wa mhusika Bogoa katika hadithi (alama 4)

**AU**

7. ***Mame Bakari***

**"**Una nini ? Umeshtuka mwanangu !Unaogopa?Unaogopa nini?"

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)
(b) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo. (al.2)
(c) Eleza sifa za mrejelewa. (al.6)
(d) Eleza umuhimu wa msemaji. (al.4)
(e) Tambua maudhui yanayojitokeza katika kifungu hiki. (al.1)
(f) Fafanua maudhui katika swali la (***e)***kwa kurejelea hadithi nzima. (al.3)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI.**

**8. Soma makala yafwatayo kisha ujibu maswali yafwatayo**

Hapo zamani za kale, paloindokea mtu mmoja kwa jina mzee Kata. Mzee Kata alikuwa na wake wawili. Mke wa kwanza aliitwa Neema na wa pili aliitwa Nduli. Kila mmoja wa wake hawa alikuwa na mtoto mmoja. Neema alikuwa na mtoto wa kike kwa jina Majaliwa. Majaliwa alikuwa ameumbwa akaumbika.Uso wake ulihimili macho meupe mfano wa theluji. Meno yake ya juu yalipangika kwa njia ambayo iliyafanya kuacha mwanya ambao ulifanya tabasamu yake kuwa ya mvuto wa sumaki. Urembo wa Majaliwa, kama walivyosema wengi, ungemtoa nyoka yeyote pangoni.

Kwa upande mwingine Kutu, bintiye Nduli, alikuwa mwenye sura mbaya ya kutisha.Uso wake usiopendeza ulimfanya kuonekana kama ajuza wa miaka mia moja! Tabia yake ya ukorofi ilikoleza mvuto wake hasi. Vijana wa kijijini walimfanyia inadi kila mara kwa kumkumbusha kuwa hakufaa kuringa. "Sura kama kiboko", wangemtania
Tofauti za kiumbo kati ya Majaliwa na Kutu zilizua uhasama mkubwa kati ya ndugu hawa, sikwambii mama zao. Hali hii ilizidishwa Zaidi na nongwa za kila siku zilizotokana na ukewenza. Familia yam zee Kata ikawa medaniya vita vya wenyewe kwa wenyewe.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Hali ya mtafaruku iliendelea kuikosesha nyumba yam zee kata amani. Asubuhi moja, Mzee Kata aliamka kama kawaida yake, alijikohoza kama isharaya kutangaza kufika kwake. Daima hakupenda kuzungumza na wakeze asubuhi na mapema. Aliamini kuwa wangemletea nuksi. Kinyume na siku nyingine, mzee Kata hakuitikiwa. Ilibidi kujikaribisha nyumbani mwake. Mara tu alipovuka kizingiti cha kijumba hicho, alitupa macho yake juu yakitanda cha mayoweambapo mke wake alijinyosha twaa kakauka kama ukuni; hanapumzi. Weupe wa macho yake na mapovu yaliyomtoka kinywani yalimhakikishia Mzee Kata kuwa Neema kampungia mkono. Harufu kali ya sumu ilihanikiza hewa kumwarifu kuwa Mzee kata kuwa mkewe kafa kwa kutendwa na mkemwenza

Maisha ya Majaliwa yalichukua mkondo mpya baada ya tanzia hii. Mama wa kambo sasa alipata mwanya wa kumhini majaliwa. Kazi zote za nyumbani aliachiwa yeye.Huku Kutu akiachwa huru kucheza. Majaliwa alipewa chakula hapa; wengine wakila biriani yeye alipewa wali wa kawaida. Mavazi yake yaligeuka matambara.Siku zilivyozidi kusonga ndivyo mateso yalivyoongezeka. Mama wa kambo alizidisha wivu wake kwa majaliwa. Hata Majaliwa alipovunja ungo na wachumba kuja kumposa, mama wa kambo aliwafukuzia mbali. Wenine walihimizwa kumposa Kutu. Wachumba waliochachawa kutaka kumuoa majaliwa wakidai kuwa hawamtaki Kutu kwa sababu ya kiburi chake, walinyeshewa matusi, wakahizinika na kujiendea zao.

Siku moja alitokea kijana mmoja makini .alikuja amavalia gwanda jeusi lililojiinamia kwa uchovu. Viatu alivyovaa vilikuwa vimejichokea kwa kupiga lami. Kofia iliokuwa kichwani pake ilitosha kumhakikishia mama wa kambo kuwa huyu alikuwa fakiri. Mama mtu alikubali mara moja posa ya kijana huyu kwa Majaliwa akijua kuwa angeadhibika. Aliamini amemtokomeza Majaliwa ndani ya lindi la ulitima. Mzee Kata naye hakusita kumwoza Majaliwa kwa kiajana huyu maana aliiona hii kama fursa ya pekee ya kumwepusha vitimbi vya mama wa kambo

Majaliwa aliandamana na mume wake hadi Kijiji cha peponi ambako kijana huyu allishi. Wallingia katika nyumba ya msonge ambamo Majaliwa alitarajia kuanza Maisha ya ndoa. Walitayarisha chajio, wakala na kulala.
Asubuhi, Majaliwa aliamshwa na nyimbo za ndege. Alipofunguamacho, alijikuta kalala ndani mya chumba chenye sakafu ya vigae. Ukuta wa chumba hicho ulikuwa wa rangi wa zari. Mapambo ya dhahabu yalitundkwa ukutani. Kumbe kijana aliyemuoa hakuwa maskini kama ilivyodhaniwa! Alikuwa mwana wa mfalme! Na hili lilikuwa kasri hasa! Majaliwa hakueza kuamini! Alikuwa ameamkia Maisha ambayo hakuwahi yawazia.

Alipoingia sebuleni alimpata mama yake mpenzi, akiwa na tabasamu ya milele usoni. Walikumbatiana kwa shauku kuu. Kumbe kijana huyo alikuwa ametumwa na mamake Majaliwa! Mumewe majaliwa alishuhudia kwa umbali. Machozi ya mama mtu na mwanawe yakilovya vifua vyao na kuyeyusha simanzi na kuyeyusha simanzi iliyokuwa imeyaandama Maisha yao. Tangu siku hiyi, watu hawa wallishi kwa raha mstarehe. Hadithi yangu inaishia hapo.

<u>MASWALI</u>

a) Taja na utolee mifano mbinu sita za kimtindo zilizotumiwa katika utungo huu (al.3)
b) Utungo huu unaweza kuainishwa kama ngamo, toa sababu (al.1)
c) Fafanua umuhimu nne wa formula ya kumalizia katika utungo huu (al. 4)
d) Taja shughuli moja ya kijamii katika jamii ya utungo huu (al. 1)
e) Jadili tatizo moja la ukewenza katika utungo huu (al.1)
f) Taja na ufafanue dhima tano ya utungo huu katika jamii yake (al.5)
g) Taja mambo mawili ambayo fanani anaweza kutekeleza ili kuufanya utungo huu uwe wa kuvutia Zaidi (al. 1)
h) Miviga ni nini? (al.1)
i) Taja hasara tatu za miviga (al.3)

–

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

–
–
–
–
–
–

–
–
–
–
–
–
–
–
–
–
–
–
–
–
–
–
–

**MTIHANI WA PAMOJA YA CASPA**
**HATI YA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI 102/1**
**KISWAHILI KIDATO CHA NNE**

**Karatasi ya 1**

1. Umechaguliwa kuwa katibu wa Chama cha Kiswahili shuleni. Andaa kumbukumbu za mkutano uliofanyika hivi majuzi ili kupanga mikakati ya kukiendeleza Kiswahili ndani na nje ya shule yenu.

2. Vijana wa sasa wanakumbwa na changamoto nyingi za maisha. Thibitisha kauli hii huku ukieleza namna wanavyoweza kuzishughulikia.

3. Ngozi ivute ili maji.

4. Andika insha itakayomalizikia kwa kifungu hiki:-
…….. ndivyo wahenga kuwa aliye juu mngojee chini. Hii ni zamu yao sasa. Wamewadhulumu wanawake kwa miaka na miaka. Wacha wapate kichapo cha kisasi.

**CASPA**
**MTIHANI WA PAMOJA WA JIMBO LA PAROKIA YA AMUKURA**
**CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA SEKONDARI KENYA**
**102/2**
**KISWAHILI – KARATASI YA 2 -LUGHA**

**1. Ufahamu (Alama 15)**
***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata***

Wahenga walisema kutoa ni moyo usambe ni utajiri. Iwapo wangefufuka leo hii wangeongezea kuwa ujasiri ni moyo usiseme ni umri. Kauli hii kama ile ya kwanza imesheheni ujumbe muhimu. Katika jamii nyingi, mtoto haruhusiwi kukaa au kuzungumza mbele ya watu wazima. Ni ajabu basi kwa mtoto wa kike kutoka jamii yenye imani kali za jadi zinazomdunisha mwanamke kuweza kupata tuzo yenye staha ya juu zaidi.
access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Malala Yousafzai alishinda Tuzo ya Nobel mwaka 2014 akiwa na umri wa miaka 17. Aliyeshinda naye tuzo hii adhimu ni Kailash Satyarthi. Kigoli huyu alituzwa tunu hii kwa kupigania haki za wasichana kupata Elimu nchini Pakistan. Harakati hizi hakuzianza juzi. Mwaka 2012 alipigwa risasi na mijibaba ya ugaidi ya kundi Fulani linaloegemea mrengo wa siasa kali kwa 'hatia' za kuwatetea mabanati. Inasemekana alishambuliwa alipokuwa akisafiri kwenye basi la shule. Kilichochochea mashambulizi ni tuhuma kuwa alikuwa ameanzisha jukwaa kwenye mtandao wa Shirika la Utangazaji la BBC alilokuwa akichangia maandishi alipokuwa na umri wa miaka 11. Maandishi yake yalikuwa na ujumbe wa kupinga juhudi za makundi Fulani kuwanyima wanawake Elimu.

Haikuwezekana hata baada ya kupona kurudi Pakistani. Alihamia Uingereza alipofadhiliwa na wahisani. Licha ya kuwa aliishi ugenini na bila aila yake mwana huyu hakupoteza makali ya ari yake ya kuendelea kutetea maslahi ya kielimu ya wenzake wa kike.

Yeye ndiye mwenye umri wa chini zaidi katika historia kupata tuzo hili. Baadhi ya wale walioshinda Nobel katika umri mkubwa ni Desmond Tutu, Nelson Mandela na Wangari Maathai. Kila mmoja wao alitambuliwa kwa sababu mahususi zinazohusu jitihada za kuboresha maisha ya wanajamii.

Njia nyingine kuu aliyoitumai Malala ni hotuba. Mwaka 2013 alihutubia Kongamano la Vijana la Umoja wa Mataifa katika hafla iliyoandaliwa kwa heshima yake. Aliwashangaza wengi kwa ufasaha na uweza wake wa kutongoa hoja. Kila mtu aliguswa na dhati ya kauli zake. Katibu Mkuu hakuwa na jingine ila kulipa kongamano hilo jina Malala. Mtoto huyu wa kimaskini alipewa taathima ambayo watu wachache sana wamepata kutunukiwa. Hii ni heshima inayotengewa marais na wafalme. Na wanapoipata huruhusiwa kuhutubia kwa dakika tano tu.

Mwaka 2014, viongozi wenye sifa za ubabe wa kuwabinya wapinzani wao lakini wameshindwa kuwaokoa wanyonge walipokuwa wakilaza damu, yeye alisafiri hadi Naijeria kudai kuachiliwa kwa wasichana 200 waliotekwa nyara na kundi haramu.

Katika hotuba iliyojaa hisia ambazo huhusishwa tu na akina mama wenye uzazi mkubwa aliyoitoa Naijeria , aliwaasa watoto wenzake wasimruhusu mtu yeyote awaambie kuwa wao ni wanyonge au hawana uwezo. Aliwanasihi kuwa wao sio wadhaifu kuliko wavulana na wasijione wanyonge kuliko watoto wa kitajiri wala wale wanaotoka nchi zenye uwezo mkubwa . Alihitimiza kuwa wao ndio watakaoijenga jamii na kuwa wana uwezo wa kuyaendesha mambo.

Mshindi wa tuzo hii yenye thamani ya dola za kimarekani milioni moja ameitabaruku kwa watoto wenzake ulimwenguni. Bila shaka mwanzilishi wa tuzo ya Nobel ameguswa na tendo la mtoto huyu huko kuzimuni. Kama kumbukizi tunu hii hutolewa wakati wa kuadhimisha kifo cha Mwanaviwanda wa

Kiswidi aliyeasisi tuzo hii kufuatana na wosia wake mwaka 1895. Kama Alfred Noble mwenyewe, kwake Malala, ngwenje au darahimu si muhimu . Lililo muhimu ni ukombozi wa watoto na hasa wa kike kielimu. Malala bado anavaa mtandio wake huku akidhihirisha adabu na unyenyekevu wa kupigiwa mfano.

## Maswali

1. Eleza mtazamo wa jamii ya Malala kuhusu watoto wa kike. (alam.2)
2. Unafikiri Malala alistahili kutuzwa Tuzo ya Nobel? Toa sababu tatu. (alama.3)
3. Ni njia zipi alizozitumia Malala kutetea haki ya watoto wa kike kupata Elimu? (alama 3)
4. Malala anawapa ushauri upi watoto wenzake? (alama. 1)
5. Kwa nini inasemekana kuwa Tuzo ya Nobel ina staha ya juu zaidi? (alama.2)
6. Andika kichwa kifaacho kwa kifungu hiki. (alama.2)
7. Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa: (alama. 3)
   a) Tunu
   b) Wahisani
   c) Ubabe

2. **UFUPISHO**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Ukame ni tukio hatari la kimaumbile. Athari zake hutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine. Kwa sababu hiyo, si rahisi kuielewa dhana ya ukame; kwa hakika si rahisi kuifafanua dhana hii. Katika eneo la Bali, kwa mfano, isiponyesha kwa muda wa siku sita wenyeji huchukulia hali hiyo kuwa ukame japo kiasi hicho cha mvua ni kikubwa mno ikilinganishwa na Libya ambayo hupata kiasi kidogo cha chini ya milimita 180 ya mvua kwa mwaka.

access more learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Katika hali ya kawaida ukame hutokana na kipindi kirefu cha uhaba wa mvua hasa katika mzima au zaidi. Uhaba huu wa mvua huweza kusababisha uhaba wa maji kwa shughuli, kundi au sekta Fulani. Shughuli za binadamu huweza kufanya hali ya ukame mbaya zaidi.Shughuli hizo ni pamoja na kilimo, unyunyiziaji maji na ukataji wa miti.

Ni vigumu kubaini wakati mahususi ambao ukame huanza kwa kipindi hicho cha ukosefu wa mvua huwa cha mfululizo, na eneo huendelea kupata mvua iliyopungua kwa miezi au hata miaka. Mimea hukauka na wanyama hufa kutokana na ukosefu wa maji. Ukame basi huwa hatari kwa maisha ya binadamu na viumbe wengine kwa kuwa huweza kusababisha njaa na kuyafanya maeneo kuwa majangwa.

Mbali na ukosefu wa mvua, ukame pia husababishwa na kiangazi. Kiangazi huongeza kiwango cha joto. Joto hilo hufanya maji yaliyohifadhiwa kuwa mvuke haraka, hivyo kiwango chake kupungua. Hali ya *el ninyo* pia husababisha ukame katika baadhi ya maeneo ambayo huwa hayana mvua. Upepo huivutia mvua mahali panaponyesha na kuliacha kame eneo ambalo halina mvua ya aina hii. Hata katika maeneo yenye mvua ya *el ninyo* , kiangazi kikali huifuata na hivyo kusababisha ukame. Hali hii huitwa *la nina*. Mambo yanayotokana na mabadiliko ya hali ya anga ulimwenguni pia yanaweza kuchangia ya ukame. Ongezeko la joto duniani linafanya hali ya ukame kuwa mbaya zaidi.

Ukame una mdhara chungu nzima kwa binadamu. Madhara hayo huweza kuwa ya kiuchumi, kimazingira, kimazingira au hata kijamii. Ukame husababisha kupungua kwa mimea na mavuno. Huweza pia kutokea dhoruba za mchanga. Dhoruba hizi hutokea palipo na jangwa. Ukosefu wa maji ya kunyunyizia mimea husababisha njaa na magonjwa kama vile utapiamlo yanayotokana na ukosefu wa lishe bora. Makazi ya wanyama wanchi kavu na wale wa majini pia huathiriwa vibaya. Hali kadhalika, ukame husababisha uhamaji. Hii inamaanisha kuwa jamii huweza kutoka katika makazi asilia na wakati mwingine huweza hata kuwa wakimbizi.

Ukame husababisha ukosefu mkubwa wa maji. Ukosefu huu huwa na athari hasi kwa maendeleo ya viwanda kwa kuwa vingi huhitaji kiasi kikubwa cha maji. Juu ya hayo, maji huhitajika katika kuzalisha umeme. Umeme una matumizi mengi katika viwanda, nyumbani, afisini na hata hospitalini. Ukosefu wa umeme basi huwa ni tatizo kuu.

Aidha, ukame husababisha madhara mengi, binadamu wanaweza kujikinga kutokana na uhaba wa rasilimali za asili kama vile chakula na maji. Pia mioto mikubwa huweza kuenea haraka wakati wa ukame na hivyo kusababisha vifo vya binadamu na wanyama na uharibifu wa rasilimali nyingine.

Ingawa ukame husababisha madhara mengi, binadamu wanaweza kujikinga kutokana nao kwa kupunguza makali ya ukame. Jambo la kwanza wanaloweza kufanya binadamu ni kuhifadhi maji. Maji

ya mvua yanafaa kuhifadhiwa katika mabwawa na mapipa. Haya yanaweza kutumiwa wakati wa ukame hasa katika kukuza mimea. Mkakati mwingine ni kutumia mbinu za kupunguza chumvi na kemikali nyingine zilizomo kwenye maji ya bahari ili yaweze kutumika katika unyunyiziaji wa mimea. Hili litapunguza tatizo la ukosefu wa chakula. Pia ni muhimu kufanya utafiti kuhusu hali ya anga ili kupanga na kuweka mikakati ifaayo kukabiliana na hali hiyo.

Ni muhimu kuwa na mipangilio mizuri ya matumizi ya ardhi. Mathalani upanzi wa mimea itakayozuia mmomonyoko wa udogo, kubadili aina ya mimea inayokuzwa sehemu fulani pamoja na upanzi wa mimea isiohitaji mvua nyingi katika kame ni hatua mwafaka. Aidha, ni vizuri kupunguza matumizi ya maji hasa katika mazingira ya nyumbani kwa mfano tunapofua na kuosha. Njia nyingine ya kukabiliana na tatizo hili ni kusafisha maji yaliyotumiwa ili kuyatumia tena.

(a) Kwa maneno **50**, eleza visababishi vya ukame kwa mujibu wa taarifa (alama. 4; 1 ya mtiririko)
**Matayarisho**
**Nakala safi**

b) Fupisha ujumbe wa aya ya **tano** hadi **saba** kwa maneno 70. (alama. 6; 1 mtiririko )
**Matayarisho**
**Nakala Safi**

**c)** Eleza masuala ambayo mwandishi ameibua katika aya mbili za mwisho kwa maneno **60**.
**(alama 5; 1 ya mtiririko)**
**Matayarisho**
**Nakala safi**

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA ALAMA 40**

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

a) Andika maneno yenye miundo ifuatayo. (alama.2
- i) Kipasuo ghuna cha midomoni, irabu ya chini, kati, kipasuo sighuna cha ufizi, irabu ya juu mbele.
- ii) Nazali ya ufizi, kipasuo ghuna cha kaakaa laini, irabu ya juu, nyuma, irabu ya nyuma wastani.

b) Bainisha silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo (Alama. 1)
- i) Waliotusifia
- ii) Sherehekea

c) Andika sentensi ifuata katika wingi. (Alama.2)
Wayo wa mguu wangu wa kulia umeungua

d) Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama. 1)
Njia hii yetu inapitiwa na mtu mnene

e) Tunga sentensi moja yenye kivumishi cha pekee kinachoonyesha idadi jumla. (alama.1

f) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo
- i) Maafisa hao walipewa uhamisho. Maafisa wengine hawakupewa uhamisho
(unganisha kuunda sentensi ambatano) (alama.2)
- ii) Hadithi hiyo <u>ilitungwa</u> vizuri <u>ikawavutia</u> wengi
( badilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari kuwa nomino) (alama.2)
- iii) Tunda halitaoshwa vyema. Tunda halitalika .
(unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia ‘po’) (alama.2)
- iv) Kengewa alitoa ahadi .Wengi waliiamini ahadi hiyo. (unganisha kuwa sentensi moja inayoanza kwa . Ahadi….) (alama .2)

g) Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba kitendo kilifanikiwa kutokana na kufanikiwa kwa kingine.
(alama. 2)

h) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kielezi. (alama.2)

i) Ainisha maneno ya liyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo. (alama. 3)
<u>Mwenyewe hakuwa amekupa</u> ruhusa kuitumia

j) Akifisha sentensi ifuatayo.
Kiwango cha umasikini katika kaunti ya homabay kinasikitisha sana itabidi sote wakatizi wa hapa tujizatiti ili tutimize malengo ya millennia seneta mteule alituhimiza

k) Andika maneno yenye mofimu zifuatazo. (alama. 2)

i) Umoja (ngeli ya u-i), mzizi, kiisho
ii) Kikanushi, kiambishi ngeli (ki-vi, Umoja)
Mzizi, kauli tendeka, kiisho

l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama. 2)
KN (N+RH) + KT (T+RE)

m) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kukanusha . (alama. 2)
Ngoma hizo zilihifadhiwa ili ziuzwe mjini.

n) Andika sentensi ifuatao katika wakati uliopita hali ya mazoea. (alama.2)
Ekapolon atawashauri wanafunzi kuhusu umuhimu wa kufanya bidii

o) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendesha kwa kuzingatia maneno yaliyopigiwa mstari (Alama. 2)
Alimfanya mtoto <u>anywe</u> uji ukamfanya <u>ashibe.</u>

p) Tunga sentensi ukitumia mzizi, ingineo kumaanisha "mbali na". (Alama. 1)

q) Hewala ni kwa kukubaliana na jambo, ……………………… .ni kwa kutoka kitu kinusurike, na…………….ni kwa aliyefanya vyema katika jambo. (alama.1)

r) Zito ni kwa jepesi, ……………………..ni kwa choyo na, ……………………ni kwa kali. (alama.2)

s) Andika visawe vya kauli zi zilizopigiwa mstari.
Atyang <u>alikumbwa</u> na matatizo mengi lakini <u>hakukata</u> tama.

4. **ISIMU JAMII**. (Alama.10)
Eleza sababu tano zinazowafunga watu kufanya makosa ya kisarufi katika mazungumzo.

**KISWAHILI KIDATO CHA NNE**
**MTIHANI WA PAMOJA WA CASPA-AMUKURA 2021**
**KISWAHILI – FASIHI**

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**<u>SEHEMU YA A</u>**
**<u>FASIHI SIMULIZI</u>**

1. Lazima
Tumia kifungu kifuatacho kujibu maswali yanayofuata

a) Nyumbani mwetu mna papai lilioiva lakini siwezi kulichuma – ndugu wa kiume asimuoe nduguye wa kike.
I) Bainisha kipera kinachorejelewa (Al 1).
II) Andika shughuli moja ya Kijamii na moja ya Kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utingo huu. (Al 2)
III) Eleza dhima nne za kipera kinachorejelewa katika jamii yako. (Al 4)
IV) Wewe ni mwasilishaji wa kipera hiki jukwani. Eleza mambo matano ambayo utazingatia katika uwasilishaji wako. (Al 5)

b) Fafanua majukumu yoyote manne ya nyimbo katika jamii. (Al 8)

**<u>SEHEMU B</u>**
**<u>TAMTHILIA</u>**

2) Tathmini maudhui ya ndoa kwa mujibu wa tamthilia ya kigogo. (Al 20)

3). "Asante ya punda kweli ni mateke, sikujua ungekuja kunihangaisha hivi".
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Al 4)
b) Fafanua tamathali ya usemi katika dondoo hili (Al 2)
c) Kauli hii ina maana gani kwa mujibu wa muktadha huu (Al 2)
d) Onyesha jinsi anayeambiwa maneno haya anavyoangaisha mzungumzaji. (Al 4)
e) Jadili jinsi hali ya "Asante ya punda ni mateke" inawaafiki wanasagamoyo. (Al 8)

**<u>SEHEMU C</u>**
**<u>RIWAYA</u>**

4. Eleza ufaafu wa anwani ya chozi la heri (Al 20)

5 a. "uuuui! Uuuui! Jamani tusaidieni! Uuuui! Uuuui! Mzee kedi usituue, sisi tu majirani! Maskini wangu!"
a) Elezea muktadha w dondoo hili. (Al 4)
b) Fafanua tamathali ya usemi huu (Al 2)

c) taja mambo yaliyofanyikia Ridhaa awali ya kuashiria mikasa. (Al 4)

b) Kwa kurejelea riwaya ya chozi la heri jadili dhiki za wakimbizi. (Al 10)

**SEHEMU D**

**HADITHI FUPI - TUMBO LISILOSHIBA**

6 a) elezea misiba inayoikumba jamii ya, "shogake dada ana ndevu" ni ya kujitakia. Thibitisha (Al 10)

b) Jadili madhila ya raia wanaoishi katika mitaa ya mabanda urirejelea hadithi ya ndoto ya mashaka. (Al 10)

7. "Maswali ya sampuli hiyo yanafaa kuulizwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Al 4)

b) Fafanua sifa tatu za msemaji wa dondoo hili (Al 6)

c) Tadhmini namna maudhui ya utabaka yanavyojitokeza katika hadithi ambamo dondoo hili limetolewa (Al 10)

**SEHEMU YA E**

**USHAIRI**

**8. Soma shairi kisha ujibu maswali**

Ndugu ona mbwa yule, ambaye ananyekenya;
Yaone mabuu yale, ambayo yamchezeya;
Kuwa leo yuafile, mwili yanautaniya;
Jana awile jasiri!

Juzi shujaa awile, pasiwe kumfikiya;
Kwenye makani yale, alipojisururiya;
Leo kuwa yuafile, mainzi yamchekeya;
Jana awile Jasiri!

Mijino mikubwa ile, ambayo 'mejitokeya;
Yali kiwaliza wale, karibu walosogeya;
Tena akibweka yule, waoga walijinyiga;
Jana awile jasiri!

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Kamwe kuishi milele, kupe ukajinyonyeya;
Walo chini yako wale, muhali unawaziya;
Ameshindwa yule pale,sembuse wewe sikiya;
Jana awile jasiri!

Kama walo hai wale, yafaa kuzindukiya;
Ni dunia maji male, muhimu kujiwaziya;
Wazipunguze kelele, na kwingi kujishauya;
Jana awile jasiri!

a) Fafanua ujumbe wa shairi hili (Al 2)

b) Eleza muundo wa shairi hili (Al 5)

c) Eleza toni ya shairi hili (Al 2)

d) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia (Al 3)

i) Ruwaza ya mistari

ii) Ruwaza ya vipande

iii) Ruwaza ya mizani

e) Eleza mbinu nne ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (Al 4)

f) Bainisha sifa mbili za anayezungumziwa katika shairi hili (Al 2)

g) Eleza tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili (Al 2)

Au

**9. Soma shairi kisha ujibu maswali**

**Nizike Ningali Hai!:** Hassam Muchai

Kipusa Binti Hamadi, siku n'takuwa kimba
Nizikwe Kifudifudi, na yoyo kuyumbayumba
Takuwa bure biladi, matozi ungayasomba
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

Tena ningaumwa ungo, na mapumu kuugua
Lioze ini na nyongo, na pua zisipumua
Takuwa sina kinyongo, mradi nimeshatua
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

Nizike sasa mwenzangu, nizike ningali hai
Singojee kufa kwangu, uanze kurairai
Kulilia kifo change, ni bure hakukufai
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

Nikifa hutonizika, kimwana sanda nunua
Manukato ya kupaka, na nguo za kuanua
Nivishe sione shaka, Washindwe kupambanua
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

Tena nikande misuli, nikande pande kwa pande
Siate kiwiliwili, shingo, miguu ikande
Umalizapo kiwiliwili, mwenzangu niende shonde
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

a) Dhamira ya matunzi wa shairi hili ni gani? (Al 2)
b) Bainisha nafsineni katika shairi hili (Al 2)
c) Eleza toni ya shairi hili (Al 2)
d) Changanua muundo wa shairi hili (Al 5)
e) Fafanua maana ya kibwagizo cha shairi hili (Al 2)
f) Eleza mbinu nne ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (Al 4)
g) Bainisha bahari ya shairi hili (Al 3)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**MURANG'A SOUTH**
**102/1**
**KISWAHILI Karatasi ya 1**
**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**
**DEC 2021**

1. Umetangazwa kuwa mwanafunzi bora katika mtihani wa kitaifa. Mwalimu Mkuu wa shule ya upili ya Tujitahidi amekualika katika shule hii yake kuwahutubia wanafunzi kuhusu kilichochangia ufanisi wako. Toa hotuba yako.

2. Ufisadi umekuwa tatizo sugu katika nchi ya Kenya. Jadili kuhusu madhara yake huku ukipendekeza njia za kuukabili.

3. Tunga kisa kitakachodhirisha maana ya methali:
   Ukiona vyaelea vimeundwa.

5. Tunga kisa kitakachomalizika kwa: . . .Hapo ndipo nilipotambua kuwa ukitenda wema umetendea nafsi yako.

**MURANG'A SOUTH**
**MTIHANI WAMWISHO WA MUHULA WA PILI**
**102/2**
**KISWAHILI KARATASI YA PILI**

**UFAHAMU:**( Alama 15)
*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Meli alipokivuka kizingiti cha lango la shule ya kitaifa ya Tungambele alikuwa na azma ya kusoma kwa bidii ili kuinukia kuwa kijana wa kutegemewa na jamii yake. Alikuwa kalelewa katika familia yenye pato wastani. Akasoma kwa juhudi za wazazi wake hadi darasa la nane alipokwangura alama za kumwezesha kujiunga na shule hii ya kifahari. Meli alijua kwamba alikuwa mwanagenzi, si katika masomo ya shule ya upili tu, bali pia katika maisha ya jijini ambamo shule hii ilipatikana. Kwa kweli hii ndiyo ilikuwa mara yake ya kwanza kutia guu kwenye jiji hili ambalo habari zake akizisoma, ama katika magazeti machache yaliyowahi kufika kijijini, au kupitia somo la Elimujamii. Hata hivyo, Meli hakuwa mtu wa kuogopa au kunywea machoni mwa changamoto. Alijiambia kwamba kwa vyovyote vile atapambana na maisha haya mapya.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Saa mbili kamili asubuhi ilimpata Meli kapiga foleni katika afisi ya kuwasajili wanafunzi wageni. Wasiwasi wa aina fulani ulianza kumnyemelea alipotazama hapa na pale bila kuona dalili ya mja yeyote aliyemfahamu. Alijihisi kama yule kuku mgeni ambaye mwalimu wake alishinda kuwaambia kuwa hakosi kamba mguuni. Hata hivyo aliupiga moyo wake konde na kujiambia kuwa kuja kwake hapa kulitokana na juhudi zake mwenyewe na katu hatauruhusu ugeni wa mazingira kuifisha ari yake ya masomo.

Usajili ulikamilika, naye Meli na wenzake wakajitosa katika ushindani wa kimasomo jinsi waogeleaji wajitumbukizapo kidimbwini wakapiga mbizi, baadhi wakiambulia ushindi na wengine wakifedheheka kwa kushindwa. Meli na wenzake walibainikiwa kwamba wote walikuwa mabingwa kutoka majimbo na wilaya zao. Ilimbidi kila mmoja wao kujikakamua zaidi ili kuelea katika bahari hii ya ushindani. Muhula wa kwanza ulishuhudia kishindo cha Meli kubwagwa chini na majabali wenzake. Alijipata miongoni mwa wanafunzi kumi wa mwisho; au kama alivyozoea **kuwatania** wenzake katika shule ya msingi, "wanafunzi kumi bora kuanzia mwisho"! Hili lilimwatua moyo Meli na kumfanya kutahayari. Alifika kwao amejiinamia kama kondoo aliyeumia malishoni. Akawataka wazazi wake wambadilishie shule lakini wakakataa.

Muhula wa pili na wa tatu mambo yalikuwa yaleyale. Meli akahisi kama askarijeshi aliyeshindwa kabisa kutambua mbinu za kuwavizia maadui. Akaona kwamba njia ya pekee ni kujiunga na wenzake kama yeye katika vitendo vya utundu kama vile kuvuruga masomo kwa kupiga kelele darasani, kupiga soga bwenini na hata kuvuta sigara. Mwanzoni alichukia vitendo hivi lakini alimeza mrututu akisema kwamba ndiyo njia ya pekee ya **kujipurukusha** na aibu. Wazazi wa Meli hawakusita kutambua mabadiliko katika hulka ya mwanao. Wakajaribu kumshika sikio nyumbani lakini akawa hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Wakawahusisha wataalamu wa ushauri nasaha ambao waliwaambia kuwa Meli hakuwa na tatizo lolote la kuyadumu masomo. Kile alichokosa ni kujiamini tu.

Wazazi wa Meli waliona kuwa ni muhimu kuwahusisha walimu katika kutatua tatizo la mwanao. Mwanzo wa muhula wa pili uliwapata wazazi hawa afisini mwa naibu wa mwalimu mkuu. Mazungumzo kati ya wazazi, naibu wa mwalimu mkuu na mwalimu wa darasa la Meli yalidhihirisha kwamba walimu walikuwa wamemuasa Meli kuhusu kujiingiza katika makundi yasiyomfaidi lakini rai zao ziliingia katika masikio yaliyotiwa nta. Aliyopenda Zaidi Meli ni shughuli zilizomtoa nje ya shule kama vile tamasha za mziki, ukariri wa mashairi na drama. Mazungumzo yalibainisha kwamba Meli alihitaji ushauri na uelekezaji Zaidi kutoka kwa mtaalamu wa nasaha pale shuleni.

Meli alianza vikao na mtaalamu huyu ambaye pia alimpendekezea Meli ushauri zaidi kutoka kwa washauri marika. Hili lilimchangamsha zaidi Meli kwani aliwaona hawa kama wenzake waliojua changamoto zake. Juhudi za mtaalamu wa nasaha na washauri marika zilifua dafu. Mwisho wa kidato cha pili ulishuhudia mabadiliko makuu katika hulka na utendaji kimasomo wa Meli. Aliukata kabisa uhusiano wake na marafiki waliompotosha na kuanza kuandamana na wanafunzi waliotia juhudi masomoni. Polepole alama zake ziliimarika. Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne yalimweka kwenye safu ya wanafunzi bora zaidi nchini.

a) "Wanafunzi wawapo shuleni hukumbana na changamoto nyingi". Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hoja sita kutoka kwenye taarifa. . (alama 6)
b) Eleza mchango wa washikadau mbalimbali katika kumsaidia Meli kupata ufanisi masomoni. (alama 4)
c) Bainisha mbinu **tatu** za lugha ambazo msimulizi anatumia katika kuwasilisha ujumbe wake katika kifungu. (alama 3)
d) i. Andika kisawe cha '**kijipurukusha**' kwa mujibu wa taarifa (alama 1)
   ii. Andika maana ya '**kuwatania**' kulingana na taarifa. (alama 1)

## 2 UFUPISHO (ALAMA 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Tangu kuripotiwa kwa maambukizi na vifo kutokana na Tandavu la Korona nchini Kenya, Wakenya wengi wamekuwa wakiishi kwa hofu. Vifo vinavyohusishwa na ugonjwa huu hatari vimekuwa vikiongezeka kila kukicha.
access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
Ugonjwa huu sugu unawafisha watu kwa muda mfupi baada ya kuambukizwa. Kutokuwepo kwa dawa za kutibu ugonjwa wenyewe kunaongeza wasiwasi miongoni mwa wanajamii. Nchi ya Kenya kama ilivyo mataifa mengine ulimwenguni imehimiza raia wake kupata chanjo dhidi ya tandavu hili. Hata hivyo, hatua ya serikali kutumia vitisho ili kuwashinikiza watumishi wa umma kupata chanjo ya korona haifai kwani huenda ikatatiza mpango wa kuchanja watu milioni kumi mwaka huu. Licha ya serikali kujaribu kuwalazimisha watumishi wa umma bado chanjo haijakubalika na wengi nchini. Kutokubaliwa kwa chanjo hii kumesababishwa na ukosefu wa elimu ya kutosha kuihusu. Watu wengi wanahofia kuwa huenda waliochanjwa wakapata madhara baadaye.

Mamilioni ya watu wameathiriwa kwa njia moja au nyingine na ugonjwa huu. Kenya imeshuhudia hoteli nyingi za kifahari kufungwa. Hii imetokana na usafiri wa ndege kusitishwa kote duniani. Kutokana na hali hiyo, hoteli zilizotegemea wateja watalii zilisimamisha shughuli zake kwa muda. Kwa mfano, ya *Intercontinental* ilifunga milango yake kabisa mwaka wa 2020. Jambo hili liliwafanya watu wengi kupoteza ajira.

Usafiri wa umma umekumbwa na changamoto si haba kutokana na tandavu la korona. Serikali ilipunguza wasafiri katika magari ya abiria kwa thuluthi moja. Wasafiri hao walilazimika kulipa nauli maradufu kwa safari ile ile. Watu wengi walilazimika kufutilia mbali mipango yao ya usafiri. Kafyu vile vile iliathiri usafiri huu wa umma. Magari mengi yalilazimika kusitisha safari njiani kwa kupatikana na kafyu. Wafanyabiashara katika sekta ya matatu wanahesabu hasara kubwa kwa kukosa abiria. Wengine wamelazimika kuuza magari yao kwa kutamaushwa na changamoto iliyowakumba ghafla.

Aidha, shule zililazimika kufungwa mnamo Machi 2020. Wanafunzi walikaa nyumbani hadi Januari 2021. Hii iliharibu kalenda ya masomo nchini. Serikali ilijaribu kuwasihi walimu kufunza mtandaoni lakini hii haikufaulu hata. Wanafunzi wa kike kadhaa waliishia kupata ujauzito hivyo basi kukatiza masomo yao. Ibada zote pia zilisitishwa. Nao waumini hawakusazwa. Baada ya serikali kufunga makanisa, misikiti na vyumba vingine vya ibada, waumini wengi walilazimika kufuatilia ibada zao katika runinga au mtandaoni. Waliokosa mitandao waliomba na jamaa zao na wengine kupuuza ibada hizo kwa muda.

Shida zilizindikana ugonjwa wenyewe ulipozidi kuenea. Hospitali za umma zililemewa na idadi ya wagonjwa waliokuwa wakienda kule kutafuta matibabu. Vitanda vilijaa na hata wengine wakalala chini katika wadi

mbalimbali. Huduma za afya zikazidi kudidimia kutokana na ukosefu wa wahudumu wa afya na vifaa vya kutumiwa na wagonjwa. Vifo vingi vikaripotiwa katika hospitali hizi za umma. Kila sehemu nchini ikaathirika. Majonzi yakajaa kila mahali.

Licha ya haya mabaya yote yaliyokuja na ugonjwa huu wa corona, kuna wale waliochuma riziki kwa kuzuka kwa ugonjwa huu. Mambo mapya yalijitokeza katika ulimwengu wetu. Msamiati wa lugha ukaongezeka. Hii ilitokana na haja ya kuwepo kwa istilahi au misamiati ya kufafanua hali mpya iliyoibuliwa na tandavu hili. Vilevile Kutokana na watu kulazimika kufanya kazi nyumbani, ujuzi wa matumizi ya mtandao umeimarika. Kwa mfano, ufundishaji mtandaoni umefaidi vyuo vingi vinavyofundisha masomo ya mbali.

Wanabiashara wengine wakaanza kuuza barakoa. Barakoa ilikuwa kitu kigeni huku kwetu na duniani kwa jumla. Wengi walipata faida kubwa sana kwa kuwa soko la barakoa lilikuwa pana. Hata hivyo, barakoa zinazotumika na wananchi wengi hazijathibitishwa kuwa bora kuzuia korona. Hali hiyo inawafanya watumiaji wake kuwa na usalama wa bandia kwani wanaweza kuambukizwa ugonjwa wa korona kwa urahisi licha ya kuwa wamevalia barakoa hizo.

Kadhalika, viyeyushi vikaanza kutumika kwa wingi humu nchini na duniani kote. Wachuuzi wengi waliingia biashara hii na kufaidika kiasi. Wengi hawakujua viyeyushi ni nini kabla ya wakati huo. Hivi sasa hata watoto wadogo wanajua viyeyushi na kutumia kwa njia mwafaka.

Kundi lingine lililonawiri kwa korona ni hospitali za kibinafsi. Wengi wa matajiri walioambukizwa ugonjwa huu walijipeleka hospitali hizi kwa matibabu. Wenye hospitali hizo nao wakapandisha bei ya matibabu kwao. Ikawa ni biashara inayonoga kabisa. Hawakujali kuhusu wale wasio na pesa.

Korona imefanikisha juhudi za maafisa wa afya kuhimiza usafi kila mara. Hii ni kwa sababu watu wanalazimika kunawa mikono yao kila mara. Usafi huu wa mikono unapunguza visa vya magonjwa kama vile kipindupindu katika jamii. Aidha, gharama za sherehe zimepungua mno kutokana na sheria za kudhibiti idadi ya watu wanaohudhuria sherehe za mazishi au matanga. Hali hii ni nafuu kwa wale wachochole ambao wakati mwingine hulazimika kuuza kidogo walicho nacho ili kugharamia sherehe za matanga au arusi.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**2 UFUPISHO.**

a) Kwa kuzingatia aya tano za kwanza, eleza shida zilizoletwa na korona. (Maneno 100) (alama 9)
Matayarisho.
Nakala safi.

b) Fupisha aya nne za mwisho kwa maneno 60. (alama 6)
Matayarisho.
Nakala safi.

**MATUMIZI YA LUGHA.**

**a) Taja sauti zenye sifa zifuatazo. (alama 2)**
(i) King'ong'o cha mdomo:------------------------------------------------------------------------------------
(ii) Irabu ya mbele kati:------------------------------------------------------------------------------------
(iii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini:------------------------------------------------------------------------
(iv) Kikwamizo sighuna cha menoni:-----------------------------------------------------------------------

**(b) Dhihirisha miundo ya silabi katika maneno yafuatayo. (alama 2)**
(i) itwa:-----------------------------------------------------------------------------------------------------------
(ii) Mchwa:-----------------------------------------------------------------------------------------------------

c) **Tunga sentensi mbili ili kuonyesha matumizi ya kiakifishi (alama 2)**
Vifungo

**d) Tunga sentensi ukitumia: (alama 2)**
(i) Kihusishi cha ulinganisho
(ii) Kihisishi cha kinyume cha matarajio

**e) Ainisha matumizi ya kiambishi "ji" katika sentensi (alama 3)**
Jibwa hilo liliweza kujinusuru kutokana na hasira za mkimbiaji.

f) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu. (alama 2)
Waziri anasoma hotuba yake.

g) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kivumishi. (alama 2)

h) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.
Nyundo hizo zimetupwa mbali na jumba lile. (alama 2)

i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama2)
Nomino ya wingi , kivumishi kiashiria, kitenzi kishirikishi, kielezi cha kiasi jumla'

j) Changanua kwa vishale: Wale wageni wetu watakuwa wamewasili leo jioni. (Al4

k) Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi inayofuata. (Al 2)
Vibarua wamefanya hiyo kazi haraka iwezekanavyo.

l) Badilisha sentensi katika kauli iliyomo kwenye mabano.
(i) Marie alipewa zawadi yake. (tendeka) (alama 2
(ii) Tunga sentensi ukitumia kitenzi kishirikishi kipungufu katika ngeli ya KI-VI. (alama 2)

m) Tofautisha matumizi ya 'Ngali' katika tungo hizi. **(alama 2)**
Mama angali mlimani
Otiende angalisoma kwa bidi angaliishi maisha mema.

n) Andika sentensi katika wakati usiodhihirika ukitumia nomino moja ya jamii. **(alama 2)**

o) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo
Hakumjia

p) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya **baba na papa** (alama 2)

q) Methali: Haraka haraka haina baraka huambiwa mtu aliye na kasi isiyofaa katika kutenda mambo.Mtu anayepuuza shida za wenzake huambiwa aje? (Al2)

r) Biwi ni kwa taka ……………………ni kwa maji na kikuba ni kwa ………………. (alam2)

**4) <u>ISIMU-JAMII ISIMUJAMII</u>**

… Bwana Spika, ninaomba kufahamishwa kwa nini Waziri wa Biashara ameshindwa kuchukua hatua kukomesha uuzaji wa vileo hatari kwa watoto wa shule.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

(a) Fafanua sifa zozote tano za sajili inayorejelewa na maneno haya **<u>al 5</u>**

(b) Eleza mambo yaliyochangia msambao wa Lugha ya Kiswahili kabla ya kuondoka kwa wakoloni barani. Al5

**MURANG'A SOUTH**
**102/3**
**KISWAHILI – FASIHI**
**KARATASI 3**
**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI KIDATO CHA NNE**

**<u>FASIHI SIMULIZI (LAZIMA)</u>**

**1. Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali**

Umeanguka mwamba
Jabali tuloegemea
Lilotupa kimbilio
Mahasidi kutishia
Mti mkuu umegwa
Wana wa ndege wawapi?
Bila shaka hangaiko
'Metukumba makinda
Angalikuwa pamwe nasi
Maulana Mungu wetu
Swali hilo tungemuuliza
Mbona kaacha mauko?
Ngome yetu kuvamia?

Ela mwenyewe Mwenza
Ajua hatima yetu
Lilobaki kumwamini
Riziki kutuangushia

(a) Andika muktadha ambamo utungo huu unaweza kutolewa. (Al 1)
(b) Ainisha utungo huu kimaudhui. (Al 2)
(c) Taja sifa za ushairi simulizi katika utungo huu. (Al 4)
(d) Taja na utoe mifano ya mbinu za kifasihi zilizotumiwa katika utungo huu. (Al 4)
(e) Eleza changamoto nne ambazo mtafiti hukabiliana nazo anapokusanya data ya fasihi simulizi nyanjani. (Al 4)
(f) Eleza umuhimu wa mtafiti kushiriki katika ukusanyaji wa data ya fasihi simulizi nyanjani. (Al. 5)

**SEHEMU YA B – TAMTHILIA KIGOGO**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. "Udongo tungeliuwahi uli mbichi. Limekuwa donda ndugu sasa. Waliota mizizi ikakita na wakamea hata pembe".
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Al. 4)
   (b) Taja na kueleza tamathali moja ya usemi inayojitokeza kwenye dondoo hili. (Al. 2)
   (c) Eleza sifa zozote nne za msemaji wa kauli hii (Al. 4)
   (d) Dondoo hili linadhihirisha jinsi baadhi ya wanasagamoyo walivyoshiriki kuivunja jumuiya yao. Fafanua (Al. 10)

3 Tamthilia ya Kigogo inazungumza kuhusu hali halisi katika mataifa mengi ya Kiafrika. Jadili. (Al. 20)

**<u>SEHEMU C : CHOZI LA HERI</u>**
**<u>JIBU SWALI LA 4 AU 5</u>**

4. "Nyamaza wewe! Nyinyi ndio mlioturudisha nyuma miaka yote hii – mnatuhadaa kwa vishahada mnavyotupa viuoni, vishahada ambavyo ni laana kwetu, tanuri hasa linalouchoma uwepo wetu.
access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Al. 4)
   (b) Taja na utoe mifano wa mbinu mbili za lugha katika dondoo hili (Al. 4)
   (c) Fafanua madhara ya vita vya kikabila kwa mujibu wa riwaya ya chozi la heri (Al 12)
5. Maovu yametamalaki katika jamii ya Chozi la Heri. Tetea kauli hii kwa kutolea hoja kumi. (Al. 20)

**<u>6. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata</u>**

Zimepita siku ayami
Siku chungu tangu giza lipotanda
Wakati lipotazama kwa kiwewe na shauku
Pumzizo kapania, roho kupigania
Ziraili alipokakamaa aushiyo kufakamia

Nilikwita kwa sauti
Ela penzi hukunitika
Machoyo litunga mbele
Kumkabili huyu nduli
Nikabaki kunyong'onyeya
Jaala kitumainia
Mtima kujiinamia
Hatima kungojea

Ya mwisho lipopumua
Alfajiri ya kiza kikuu
Nilidhani wanichezea
Mizaha yako kawaida
Lijaribu kupulizia
Hewa toka langu pofu

Tumaini kiniambia pumzi zangu takuhuisha
Sikujua hizo likuwa juhudi za mfa maji muhebi

Macho libaki kutundiya, tabasamuyo kitaraji
Kumbe mwenzangu kaniacha!
Ukiwa ulinivaa, Ukungu ukatwandama
Pa kuegema, sikujua fundo chungu linisakama
Tabibu alipoingia na kutangaza rasmi mauko

Ilikuwa kana kwamba ndo jana lipofunga nikahi
Kumbukizi zilinijia kwa chozi telelele
Japo kifo ni faradhi ndwele hino halieleweki
Ama jicho la hasidi
Limekuangaza jamani?

Koja hili ninalokuwekea
Kando ya kasri hili la shakawa
Ni hakikisho toka kwangu, nitatamba sana na njia
Kutafuta alotuendea kinyume kutupoka
Mauko kutuleteya

**Maswali**

(a) Utungo uliosoma ni wa toni gani? Thibitisha kwa kutolea sababu mbili (Al. 3)
(b) Taja na utoe mifano ya mbinu za lugha zilizotumiwa katika utungo huu (Al. 4)
(c) Nani nafsineni katika utungo huu (Al. 2)
(d) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (Al. 4)
(e) Mishororo mishata ni nini? Toa mifano miwili katika shairi (Al.3)
(f) Eleza muundo wa ubeti wa sita (Al 4)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

7. **TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

Safari ya elimu ni kama ua la waridi ambalo licha ya upendezaji wake, huzingirwa na miiba. Jadili adha za safari hii kwa hoja tano tano kutoka kwa kila mojawapo wa hadithi fupi zifuatazo: Mapenzi ya Kifaurongo, Mame Bakari, Mwalimu Mstaafu na Mtihani wa Maisha.

**BUURI**
**KISWAHILI**
**102/1**
**KARATASI 1 102/ - INSHA**

Swali la lazima .

1. Wewe ni mkazi wa eneo la Songambele na unataka kuwania ugavana katika kaunti ya mavuno.
   Andika tawasifu utakayowasilisha kwa raia ili waweze kukuchagua.

2. Janga la Koroan limeathiri jamii kwa kiasi kikubwa. Jadili.

3. Andika kisa kitakachathihirisha maana ya methali « pilipili usioila yakuwashiani »?

4. Andika kisa kitakachoanza kwa « …………………………. « Nilikaa pale kwa Mseo wa hisia, nisijue kama nilifurahishwa ama nilihuzunishwa na kisa hicho……………….

**BUURI**
**102/2**
**KISWAHILI: LUGHA**
**(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha na Isimu Jamii)**
**KARATASI YA 2**

***MATUMIZI YA LUGHA.***

a) Andika maneno yenye miundo ifuatayo. (a.3)
   i) Kipasuo singhuna cha kaakaa laini, irabu ya nyuma kati, kilipasuo ghuna cha masine, irabu ya nyuma kati, kipasuo ghuna cha masine, irabu ya mbele juu.
   ii) Nazali ghuna ya kaakaa gumu, irabu ya chini kati, nazali ghuna ya ufisi, irabu ya mbele juu.
   iii) Irabu ya chini kati, irabu ya mbele juu, kipasuo ghuna cha mdomo, irabu ya nyuma juu.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

b) Weka shadda katika neneo lifuatalo. (al.1)
   atatutemebelea.
c) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (al.2)
   Wakija wapeni wahandisi wawili wawashughulikie.
d) Andika kwa ukubwa hali timilifu. (al.2)
   Mtego ulimnasa ndovu huyo.
e) Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha 'a' unganifu na kihusishi cha mtenda. (al.2)
f) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagaizo.
   i) Raia wakipatana maendeleo yataimarika(tumia 'po'). (al.2)
   ii) Wanakijiji walishirikiana kukomesha wizi wa mifugo(anza kwa Wizi wa Mifugo…………..) (al.2)
   iii) Taka zilijaa. Taka zilizolewa . (unganisha bila kutumia kiunganishi) (al.2)
g) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopo hali isiyodhihiriaka. (al.2)
h) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al.2)
   Mkulima aliyepanda waktati ufaao amepata mavuno mengi.
i) Tambua virai vihusishi katika sentensi ifuatayo. (al.2)
   Wengine wao waliegesha kando ya barabara iliyokarabatia na kampuni ya kichina.
j) Taja na utolee mifano matumizi mawili ya mshazari. (al.2)
k) Bainisha mofimu za neno, "Kilichonywewa" . (al.3)
l) Andika sentensi hili upya kwa kutumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. (al.2)
   <u>Umoja</u> wa jamii hiyo umewawezesha kupigana na <u>umaskini.</u>
m) Kanusha
   Asha aliwapelekea wageni chakula na akawanavya mikono. (al.3)
n) Onyesha miundo miwili katika ngeli ya "LI- YA". (al.2)
o) Ainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo. (al.4)
   wanafunzi walimwatikia mwalimu mkuu mich ya matunda nje ya nyumba yake kwa ustadi wakitumia vijiti.
p) Changanua kwa njia ya matawi. (al.3)
   Kimathi si mtiifu.
q) Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo. (al.2)

i) Alipokelewa mgeni
ii) Alipokezwa mgeni.

4. **ISIMU JAMII** **(alama 10)**

(Mdundo wa Muziki) Kina mama mpo?....................!
Kina Siste nanyi ……………… are you there? Kampuni ya platinum imewaletea mafuta mpya ya filk. Mafuta hayo yana vitamin C, Suncreen na yana marashi ya kupendeza. Ukiyatumia kwa wiki moja sura yako itakuwa kama ya kitoto kichanga. Nayo macho ya wote, waa! Yatakuwa kwako 24/7. Jinunulie! Jinunulie! Mafuta ya filk.

Mafuta ya wanawake wa kisasa.

a) Taja sajili iliyotumiwa hapa. (al.1)
b) Taja sifa nne za sajili hii. (al.4)
c) Kwa nini wakenya wengi hupenda kuchanganya na kubadili msimbo? (al.5)

**BUURI**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**

***Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yafuatayo.***

Sinisumbue akili, nakusihi e mwandani,
Afiya yangu ni dhalili, muno nataka amani
Nawe umenikabili, nenende sipatalini
Sisi tokea azali, twende zetu mizimuni
Nifwateni Sipatali, na dawa ziko nyumbani.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini
Kwa nguvu ya kirijali,mkuyati uamini
Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele Fulani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini
Dawa yake ni subili,au Zogo huauni
Zabadi pia zahali, kwa maradhi yako ndani
Au kwenda wasahili, wenyewe walo pangani
Nifuateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini.
Daktari kona mwili, tanena kansa tumboni
Visu vitiwe makali, tayari kwa pirisheni
Ukatwe kama Figili, tumbo nyangwe na maini
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani.

Japo maradhi dhahili, kuteguliwa tegoni
Yakifika Sipatali, huwa hayana kifani
Waambiwa damu kalili, ndugu msaidieni
Watu wakitamali, kumbe ndio buriani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani.

Mizimu yakupa kweli, wakueleze undani
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu dhamani
Ulete kuku wawili, wa manjano na wa kijani
Matunda pia asali, vitu vya chanoni
Nifwateni sipitali, na dawa zi mlangoni?

Maswali.

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama.2)

b) Shairi hili ni la bahari gani? (alama3)

c) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama4)

d) Kwa nini mshairi anakataa kwenda hospitali? (alama3)

e) Ni nani nafsineni katika shairi hili. (alama1)

f) Tambua toni ya shairi hili. (alama1)

g) Eleza muundo wa ubeti wa pili. (alama4)

h) Onyesha Jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumika katika shairi hili. (alama 2)

i) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi . (alama2)

i) Pangani

ii) Nenende

***<u>CHOZI LA HERI</u>***

***<u>Jibu swali la pili au la tatu.</u>***

2. "Alijiona kama mfamaji ambaye anakabiliwa na mtutumo wa mawimbi ya misibu ya mmoja baada ya mwingine"

a) Bainisha muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Eleza sifa tatu za anayerejerewa katika dondoo hili. (al.2)

c) Eleza tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hii. (al.2)

d) Fafanua masaibu yaliyomkumba mrejelewa. (al.3)

e) Huku ukitolea mifano riwayani, jadili matatizo yanayowakumba wanajamii katika ndoa. (al.8)

3. a) Eleza madhara yanayoletwa na siasa za ukabila kwa mujibu wa riwaya ya Chozi ` la Heri . (al.10)

b) Jadili jinsi ambavyo mwandishi wa riwaya ya Chozi la Heri ametumia mbinu ya majazi kufanikisha maudhui yake. (al.10)

**TAMTHLIA YA KIGOGO**.

***<u>Jibu swali la 4 au la 5.</u>***

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

4. " Nimekuja kuwakomboa………………………………….

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Kwa kutumia hoja nane, thibitisha kuwa msemewa na wenzake wanastahili kukombolewa. (al.8)

c) Kwa kutumia hoja nane, onyesha umuhimu wa msemewa. (al.8)

5. Tamthilia ya kigogo ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika. Thibitisha (alama20)

***TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE.***

***<u>Jibu swali la 6 au la 7.</u>***

***<u>SHIBE INATUMALIZA.</u>***

6. " Ndugu yangu kula kunatumaliza"
"Kunatumaliza au tunakumaliza"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Eleza jinsi kula kunavyotumaliza kwa mujibu wa hadithi. (al.6)

c) Kwa kurejelea hadithi, eleza namna maudhui ya ufisadi yanavyojitoza. (al.10)

7. Huku ukurejelea hadithi zifuatazo, eleza namna maudhui ya mapenzi na asasi ya ndoa yanavyojitokeza, (al.20)

a) Masharti ya kisasa

b) Ndoto ya mashaka

c) Mtihani wa maisha

d) Mame Bakari.

8. ***FASIHI SIMULIZI*** ***(ALAMA 20)***

a) " Mwanangu nakuomba uzingatie uandilifu maishani, uongofu ni nuru ya Mustakabali wa kila mtu………………."

i) Tambua kipera na utanzu wa tungo hili. (al.2)

ii) Kwa kutumia hoja mbili, eleza muundo wa kipera hiki. (al.2)

iii) Fafanua sifa nane za kipera hiki. (al.8)

b) Eleza vikwazo vinane vya ukuaji wa Fashihi Simulizi. (al.8)

**MTIHANI WA PAMOJA YA SAMIA**
**KIDATO CHA NNE**
**102/1**
**KARATASI YA KWANZA**

1. (LAZIMA)

Andika tahariri kwa gazeti la Alwodo ukieleza sababu za watoto wengi nchini Kenya kuingilia ajira za mapema na kuacha masomo ya sekondari. (al.20)

2. Matumizi ya tarakilishi katika shule za misingi na za upili yana uzuri na ubaya wake. Jadili. (al.20)

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali 'Cha mwenzako kikinyolewa chako kitiie maji' (al.20)

4. Adika insha itakayomalizia kwa: Nilijitazama na kujidharau kwa nini sikuwafahamisha walimu jambo hilo mapema. (al.20)

**TATHMINI YA PAMOJA YA SAMIA**
**KIDATO CHA NNE**
**102/2**
**KARATASI YA 2**
**Dec -2021**

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia</u>*.**

Nchi yetu imeraukia mawio ya machafuzi ya kisiasa baada ya shughuli za uchaguzi zilizogonga mwamba mkuu. Hili lilijiri baada ya Tume ya uchaguzi kukosa kuendeleza uchaguzi kwa njia inayostahili. Jambo hili lilizaa msukosuko wa kisiasa usiomithilishwa katika historia ya taifa letu.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Hivi sasa wakenya wanaishi kwenye kambi za watu wasio na makazi. Hiki ni kinaya kikuu kwani matukio haya yamezuka baada ya miongo minne ya uhuru. Vilio vya wakenya vimeshamiri na kupaasa sauti vikalalamikia kukosa makazi, lishe na ndoa kusambaratika. Ndoa zimevunjika baada ya'wenyeji' kuwatimua 'wageni na damu kumwagika.

Kenya imekuwa miongoni mwa mataifa yanayowapa faraja wakimbzi kutoka nchi jirani zinazokumbua na vita vya wenyewe. Vita katika Somalia vimesababishwa na koo mbali zinazopigania uongozi hali ambayo imekwamisha shughuli zote za kiuchumi.

Hali ya sasa ya Kenya imechochewa na msururu wa sababu; ukabila na tama ya uongozi zilionekana wazi katika miundo ya vyma viku vya kisiasa na katika kampeni zao. Wakenya walipiga kura kwa misingi ya kikabila upande ukitazamia mtu wao kushinda uchaguzi huo.

Kwa upande mwingine , viongozi hao kutokana na tamaa ya uongozi walikuwa wamesmua kushinda uchaguzi huo kwa vyovyote vile. Leo tunavuna matunda ya siasa za ukabila na tamaa ya mamlaka.

Maelfu ya wakenya ni makimbizi nchini na katika nchi jirani ya Uganda. Wakenya hao wanahitaji msaada wa chakula na mahitaji mengine ya kimsingi. Serikali na shirika la msalaba mwekundu zimefanya juhudi kuwasaidia wahasiriwa lakini kuna tetesi kwamba ubaguzi umejipenyeza katika ugawaji wa msaada huo.

Waliopewa jukumu la kugawa msaada huo ni sharti waelewe kuwa waathiriwa ni wakenya wenzao na hawafai kubaguliwa kwa misingi ya makabila yao. Matukio kama hayastahili asilani katika taifa hili.

Twahitaji zao <u>aali</u> la viongozi wasiojitwika ubabe bali wawe watumishi wa wananchi wanastahili kutupilia mbali tamaa za kujilimbikiza mali na kung'ang'ania uongozi. Pia katiba inafaa irekebishwe. Wakenya wanastahili kuelimishwa kuhusu undugu na utaifa. Fauka ya haya masuala yanayohusiana na hatimiliki za ardhi yanafaa <u>kutandaraukiwa kwa dhati.</u>

a) Taja madhara manne ya ukabila. (al.4)
b) Shughuli za ugawaji wa misaada zimekumbwa na changamoto gani. (al.2)
c) Eleza tofauti ya chanzo cha vita nchini Somalia na Kenya. (al.2)
d) Mwandishi anatoa mapendekesho gani ya kutatua tatizo hili la ukabila. (al.3)
e) Eleza kinaya cha maisha ya wakenya kwa sasa. (al.2)
f) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumika katika kifungu cha ufahamu. (al.2)
   i. Mawio.
   ii. Tandaraukiwa kwa dhati.

**2. UFUPISHO**

***Soma makala haya kishaujibu maswali yanayofuata.***

Tangu asili –na jadi nasikitika kusema kuwa tumekuwa tukiwakandamiza mabanati wetu na kuwateka bakunja ilhali wameonyesha kuwa mikono miepesi. Siku mojanilikuwa nikitembea na babu yangu mkongew tulipoliona tapo lawanawake kwambali. " Funika kombe mwanaharamu apite!" akininong'onezea, wanahusudu uwezo tu. " Kwa uchungu watu wa fikira sikuelewa yakini alichotazamia lakini hii leo nang'amua. Basi imenibidi kutupilia mbali dhana hiyo hafidhina kwani asifuye mvua aghalabu imemnyea.

Jina nzuri hung'aa gizani na bila shaka majina ya wanawake watu yameremeta kama nyota.
Kwanza, wamejitolea mhanga katika nyanja za masomo. Si baba ambao wamehitimu kutoka vyio vikuu vya humu nchini na vile vile vya ughaibuni na kujipa shahada kadha wa kadha. Wamepata ujuzi wa kutosha katika maswala tatizo kama vile udaktari na uanasheria. Hivi ni kumaanisha kuwa tuna madkari shupavu, basi tuwape nafasi tusiendelee kuwa nyuma mithili ya koti katika kipengele hiki muhimu cha maisha. Ni wanawake ndio, lakini mgalla muue na haki umpe!

Vile vile wanawake wenu wamejitokeza kifua mbele katika hatamu za uongozi. Mfano mwafaka katika serikali yetu, ambapo mawaziri ni wanawake. Nani asiyewafahamu, Cecily Kariuki, Racheal Omamo na Amina Mohamed? Wote wanafanya bidii za mchwa kustawi maisha ya wananchi. Ingekuwa ida na inadi kama tungewanyima viongozi hawa nafasi hizo na bila shaka jambo hili lingeathiri sana ujenzi wa taifa kwani ujuzi ndio nguzo ya kila kitu.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Kwa upande mwingine wanawake ni walezi waliomakinika.Kama tujuavyo udongo hupatilizwa ungali maji na usipoziba ufa huna budi kujenga ukuta. Nani ndio wamepokezwa jukumu mahiri la malezi? Nina zetu hujitolea kwa hali na mali kuwakuza watoto kwa tajriba zinazofaa na kuwafunza maisha ndiposa wasifunzwe na ulimwengu. Aliyemakinika atakubaliana name kuwa malezi si jambo la kufanyiwa mzaha katika harakati za ujenzi wa taifa. Na huu wajibu wote ni wa mwanamke.

Siwezi kuwasahau wanamke wanamuziki. Sote twaelewa kuwa kwa uchumi kama wetu, kutengemea kazi ya kuajiriwa ni kutaka muhali, chambilicho wahenga mchagua jembe si mkulima. Nashukuru wanadada wetu kwa kutia bidii katika uwanja wa mziki badla ya kuwa viruka njia. Kupitia kwa sauti nyororo kama kindanda wameweza kuwavutia hata watalii kuitembelea nchi yetu na kutuachia pesa za kigeni. Nawahimiza wengi kama iwezekanavyo wajaribu bahati yao…………jambo hili linajuza sana katika ujenzi wa taifa imara.

Katika kitengo cha spoti, waawake wamejizatiti vilivyo na kutokea wanashati kweli kweli.
Wamezika katika kaburi la sahau kuwa mchezo ni uawala wa wanaume. Kwa mfano katika michezo ya Olimpiki au jimuiya ya madola timu zetu za wanawake zimefanya vyema na kurudi nyumbani na nishani chungu nzima.Kwa wale wasiohusika katika michezo ningewasihi wajikakamue kisabuni basi wasiwaonee kijicho wenzao, kwani nyote ya mwenzio usilalie mlango wazi. I wapo tutazingatia ufanisi katika michezo, taifa hili halina budi kuendeleza uchumi wake.

Kwa kukunja jamvi, ningetaka kusisitiza kuwa hata ingawa jitihada haziondoi kudura, wanawake wetu wamefanya bidii za kutosha na inafaa wapewe nafasi sawa na wanaume katika ujenzi wa taifa. Ningewahimiza wanaume wasiwe na kinyongo dhidi ya wamawake bali chanda chema huvishwa pete. Huu ndio wito wangu na kama tujuavyo kuro hasemi uongo na mbiu ya mgambo ikilia haikosi ina jambo.

***MASWALI***

a) Fafanua dhima ya mwanamke kulingana na makala haya. (maneno 70-80) (al.6)
**Nakala safi**

b) Bila kubadilisha maana fupisha aya ya pili nay a tatu. (maneno 50- 55) (al.7)
**Nakala safi**

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

a) Andika maneno yanayoafiki maelezo haya: (al.2)
i. Nazali ya midomoni, kipasuo sighuna cha midomoni, kiyeyusho, irabu ya chini kati.
ii. Kipua ghuna cha kaakaa laini, irabu ya chini kati, kimadende ghuna cha ufizi, irabu ya chini kati.

b) Ainisha mofimu kwa kurejelea majukumu ya kisarufi katika neno hili. (al.3)
Alijipelekea

c) Tunga sentensi ya swali ukitumia kiwakilishi nafsi ambata nafsi ya pili wingi. (al.2)

d) Kwa kutolea mifano, andika miundo miwili ya ngeli **ya LI-YA**. (al.2)

e) Andika sentensi ifuatayo kwa udogo wingi. (al.2)
Mtoto mkaidi aliiba kitabu cha mwenzake.

f) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania katika wakati ujao hali ya kuendelea. (al.2)

g) Andika katika usemi halisi mtindo wa kitamthilia. (al.4)
Khaemba Ouma alitaka kujua ni kwa nini Wandera Otieno alipenda Hisabati, Wandera Otieno akamweleza alipenda Hisabati kwa kuwa babake alikuwa mwalimu wa somo hilo.

h) Unda nomino tatu kutokana na kitenzi **safari**. (al.3)

i) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya **daka** na **taka**. (al.2)

j) Tunga sentensi mbili tofauti kuonyesha matumizi ya lama za mtajo. (al.2)

k) Yakinisha katika umoja. (al.1)
Msipofanya bidii hamtapita mtihani.

l) Tunga sentensi ukitumia ka kuonyesha mfulilizo wa matukio ya matukio ya wakati uliopita. (al.2)

m) Unda sentensi changamano kutokana na tungo zifuatazo: (al.2)
Mtoto alikuja nyumbani jana.
Mtoto ndiye huyu.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

n) Jibu swali kulingana na agizo. (al.2)
Halima alimbebea mwalimu mzigo kwa gari. (Anza kwa yambwa tendewa)

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielezo cha visaduku. (al.5)
Kile kizuri kilikuwa kikitumika ba baba Yule

p) Tunatumia shabaha tunapofurahishwa na jambo…………………………..tunapokula kiapo na yarabil…………………… (al.2)

q) Andika maana ya maneno yafuatayo: (al.2)
i. Kula kalenda
ii. Kula njaro.

4. ISIMUJAMII. (al.10)
Janga tandavu la korona limeathiri maisha ya kila mtu duniani, umepewa nafasi kama muuguzi kuzungumza na wanafunzi kuhusu suala hii. Andika sifa za lugha utakayotumia katika hotuba yako.

**MTIHANI WA MWIGO GATUZI LA SAMIA**
**KIDATO CHA NNE**
**102/3**
**KARATASI YA TATU**
**NOV -2021**

***SEHEMU YA A: TAMTHILIA* - KIGOGO P. KEA (alama 20) SWALI LA LAZIMA**

1.
“Lisilowezekana ni kukama ndume…………hujafa hujaumbika.”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
b) Taja na ueleze mbinu moja ya lugha inayojitokeza katika dondoo hili. (al.2)
c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (al.4)
d) Jadili mbinu zozote kumi walizozitumia wanasagamoyo kujikomboa kutoka uongozi dhalimu katika jimbo la Sagamoyo. (al.10)

**SEHEMU YA B: (CHOZ LA HERI)- K. MATEI**

Jibu swali la 2 au la 3

2. Riwaya

“ Tumeendelea kuwakwaza akina dada huku tukididimiza nguzo ya jamii yetu. Na kuwe huko kumtoa mekoni, lakini hili la kumpa jukumu la kuiongoza jamii nzima! Itakuwa kukivisha kichwa cha kuku kilemba.”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
b) Eleza mifano **mitatu** ya kukwezwa kwa mwanamke na **mitatu** ya kutwazwa kwa mwamume kama anavyodai nafsineni. (al.6)
c) Jadili umuhimu wa mandhari katika kujenga riwaya hii kwa kurejelea shule ya Tangamano. (al.10)

3. “Ukiukaji wa haki za kibinadamu ni jambo la kawaida katika jamii ya Chozi la Heri. Jadili. (al.10)

**SEHEMU YA C: (TUMBO LISILOSHIBA)- ALIFA CHOKOCHO**

(Jibu swali la 4 au 5)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

4. a) **MAME BAKARI**- Mohammed Khelef Chassany

“Ubahimu naotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake.” Jadili ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya Mame Bakari. (al.10)

b) **MASHARTI YA KISASA** – Alifa Chokocho

“Hatimaye Dadi ilimbidi kuusikitikia ule uzuri ambao unapeleka kwingine wala si kwake. Na tazama ile kanzu jinsi ilivyomfika magotini kidada. Tazama anavyoiacha wazi ile miguu na miundi yake yenye kuvutia. Ndiyo, hata yeye Dadi akifuatana na mkewe Kidawa, wakipitana njiani wanawake wanaovaa hivyo huwatambulia macho. Kwa nini basi wanaume wengine wasimtumbulie macho mke wake yeye? Na Kidawa akimwona mumewe anawatumbulia macho wanawake hubwata kwa kimombo “Stop your gaze!” Na yeye humwuliza, ndio anasema nini? Na Kidawa hujibu, “Acha kudolea wanawake macho. Kwa nini wasiwe na uhuru wa kuvaa wanavyopenda? Au huelewi wanawake wana uhuru? “My dress my choice!” Lakini yeye hatimaye hujiuliza: Itakuwaje dunia iwapo watu wote (sio wanawake tu ) watavaa wanavyopenda?.

i) Jadili aina nne za taswira zinazojitkeza katika dondo hili. (al.4)
ii) Kando na taswira, tambua mbinu sita za kimtindo katika dondoo. (al.6)

Au

5. Ukirejelea hadithi zifuatazo kwenye Diwani, eleza jinsi maudhui ya umaskini yanavyojitokeza. (al.20)

i) Tumbo Lisiloshiba.
ii) Mapenzi ya kifaurongo.
iii) Ndoto ya mashaka.
iv) Mtihani wa maisha.

**6. SEHEMU YA D: (USHAIRI)**

Jibu swali la 6 au 7

**a) Shairi la kwanza**

**Soma *shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Maendeleo ya umma
Sio vitu maghalani
Kama tele vimesaki
Lakini havishikiki
Ama havikamatiki
Bei juu

Maendeleo ya umma
Sio vitu gulioni
Kuviona madukani
Kuvishika mikononi
Na huku wavitamani
Kama tama ya fisi
Kuvipata ng'o

Maendeleo ya umma
Sio vitu shubakani
Dhiki ni kwa mafakiri
Nafuu kwa mafakiri
Ni wao tu washitiri
Huo ni uistimari
Lo! Warudia

Maendeleo ya umma
Ni vitu kumilikiwa
access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
Na wanyonge kupatiwa
Kwa bei kuzingatiwa
Bila ya kudhulumiwa
Na hata kuhadaiwa
Hiyo ni haki.

Maendeleo ya umma
Dola kudhibiti vitu
Vijapo nchini mwetu
Na kuwauzia watu
Toka nguo na sapatu
Pasibakishiwe na kitu
Huo usawa.

Maendeleo ya umma
Watu kuwa na kauli
Katika zao shughuli
Vikaoni kujadili
Na mwisho kuyakubali
Maamuzi halali
Udikteta la.

Maendeleo ya umma
Watu kuwa waungwana
Vijakazi na watwana
Nchini kuwa hakuna
Wote kuheshimiana
Wazee hata vijana.

**Maswali**

a) Eleza dhamira ya shairi hili. (al.2)
b) Baininsha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. (al.2)
c) Eleza umuhimu tatu wa usambamba katika shairi hili. (al.2)
d) Onyesha jinsi maendeleo ya umma ulivyo kinaya. (al.2)
e) Eleza mambo ambayo mshairi nachukulia kuwa maendelo halisi ya umma. (al.4)
f) Tambua matumizi ya mstari mishata kwa kutolea mifano. (al.2)
g) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. (al.1)
h) Fafanua toni ya shairi hili. (al.1)
i) Andika ubeti wanne kwa lugha nathari. (al.4)

Au

*7.* ***Shairi la pili***

Joseph Kiponda : Taifa ni Ushuru

Lau kama ingakuwa, madhali tuna uhuru
Watu kodi kutotowa, na kuifanya kufuru
Vije nchi ingakuwa, taifa bila ndururu
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Hivi taifa kumea, nakuendelea mbele
Kwamba lajitegemea, haliwategei wale
Yataka kujitolea, ushuru bila kelele
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Wafanyikazi wa umma, mfano mwema walimu
Wauguzi mahashuma, daktari wahadimu
Bila hizi darahima, vipi wangalihudumu?
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Si vyema kuombaomba, kwa wageni kila mara
Huwa twajifunga kamba, na kujitia izara
Adha zinapotukumba, kujitegemea bora
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Miradi ya maendeleo, yahitaji darahima
Ndo tufikie upeo, ulio dunia nzima
Wadogo na wenye vyeo, bila kodi tutakwama
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Ushuru si kwa wanyonge, wasokuwa na uwezo
Watozwe hata wabunge, na wengine wenye nazo
Yeyote asijitenge, kodi akalipa bezo
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Kwetu kutoa ushuru, ndiko kujitegemea
Pasiwepo na udhuru, sio wa kuelea
Huwa ni kama kiguru, asenao kutembea
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

***Maswali***

a) Ujumbe unaowasilishwa katika shairi hili, una hadhira legwa. Zitaje. (al.3)
b) Kwa kutolea mifano, eleza aina tatu za idhini ya kishairi alizozitumia mshairi. (al.3)
c) Huku ukitoa mifano, taja aina tatu za takriri zinazojitokeza katika utungo huu. (al.3)
d) Fafanua bahari zinazojitokeza katika shairi hili. ( al.4)
e) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (al.4)
f) Taja mbinu tatu za kifani zilizotumika katika shairi hili. (al.3)

***8. SEHEMU YA E:(FASIHI SIMULIZI )***

**Soma kifungu kifutacho kisha ujibu maswali yanayofata.**

Basi kizito Matukio alipewa Cheo kikubwa kutokana na uchapakazi wake. Shirika alilokuwa akifanya kazi likawa na matumaini makubwa. Kizito naye badala ya kuchapa kazi akawa anajigamba na kujitapa mitaani. “Ukubwa ninaujua miye. Mimi ndiye Kizito hapa. Kizito Mzito mimi, akaringa. Akawadharau akina Wanjiku. Amina na Shikuku. Akajitosa kwenye raha bila kujali na kuvaa suti nzito alizoagizia kwa fedha za shirika. Muda si muda shirika likaingia hasara. Mwishowe ametimuliwa kazini na wazito wenyewe. Ameondoka na mkoba mzito wa madeni na fedheha: nguo sasa anavaa za matambara mazito! Jamani uzito unakowapeleka wazito.

**<u>MASWALI</u>**

a) Onyesha kwa nini kipera hiki ni soga (al.4)
b) Fafanua vipengele viwili vya kimtindo vilivyotumika katika utungo huu. (al.2)
c) Eleza matatizo utakayokumbana nayo nyanjani ukikusanya kazi ya kipera hiki (al.4)
d) Taja mifano mitatu ya ngomezi za kisasa (al.3)
e) Eleza hasara nne za miviga? (al.4)
f) Fafanua umuhimu wa misimu ya kisasa. (al.3)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

–
–
–
–
–

–
–
–

–
–

–
–
–
–
–
–
–

**MTIHANI WA MWIGO WA SUKELLEMO**
**102/1**
**KISWAHILI – KARATASI YA 1**
**DISEMBA 2021**

**MASWALI**

1. Lazima
   Wewe ni mwanahabari wa Runinga ya Wajuze. Umepata fursa ya kumhoji Katibu katika Wizara ya Usalama kuhusu mikakati inayowekwa kuhakikisha usalama katika kipindi cha mchakato wa siasa nchini. Andika mahojiano hayo.

2. Umegundua kuwa wanafunzi wengi katika shule yenu hawajihusishi katika michezo kama ilivyokuwa hapo awali. Andika makala kuhusu umuhimu wa wanafunzi kujihusisha katika michezo.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
   Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti .

4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa kauli ifuatayo:
   …. Nilijitazama na kujidharau. Kwa nini nilijiingiza katika hali hii? Nilijuta.

**MTIHANI WA MWIGO WA SUKELLEMO**
**102/2**
**KISWAHILI KARATASI YA 2**
**LUGHA**

**DISEMBA**

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**1. Ufahamu (Alama 15)**

**Soma makala haya kwa uangalifu kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Asubuhi hiyo kabla ya mrauko wa watu wengi kama ilivyokuwa ada ya wanakijiji cha Kaulizeni, Kabibi alimrausha mumewe Mzee Mori kwa lengo la kumpeleka kwenye zahanati ya pale pao – heko kwa mfumo mpya wa kiutawala uliotokana na kuanza kutekelezwa kwa katiba iliyoasisi ugatuzi na hapo kuwezesha taasisi zitoazo huduma nyingi muhimu kuletwa karibu na wananchi. Miaka michache iliyopita, wangehitajika kutumia zaidi ya saa nne kufikia kituo cha matibabu kilichokuwa karibu nao. Aidha, wangetakiwa kutumia matwana ambayo haikuwa rahisi kukodeshwa kutoka kwa mwenyewe kwa sababu ya zile barabara zilizoogopa kusakafiwa kutokana na utepetevu wa viongozi wao katika siku zilizotangulia. Chepkwony hakupenda kutesa gari lake kwa kuliruhusu kupitia barabara hizo ambazo ubovu wake ulitia fora. Magenge yaliyosongamana barabarani na mawe yaliyosimama wima ni kama yanapiga saluti yalikuwa tayari **kuhujumu** vigari vya wachochole kama yeye. Licha ya hofu hii, mara mojamoja alijitolea na kuwanusuru wanakijiji waliochungulia kaburi na akina wajawazito ambao siku zao zilikuwa zimetimia. Aghalabu, ubovu wa barabara hizi ulihakikisha kwamba wengi wao walitua mizigo yao kabla ya kuwasili katika Zahanati ya Nusura.

Leo hii, imewachukua dakika ishirini hivi, mwendo wa miguu na lau wangepata pikipiki, au 'nduthi' kama vijana wanavyoziita kwa kilugha legevu chao, ingewachukua chini ya dakika tatu kukamilisha safari hii. Mambo yametengenea kwelikweli. Ule mgao wa serikali ya kaunti kutoka kwa hazina kuu ya serikali ya kitaifa ulitumiwa kwa uwajibikaji mkubwa na gavana wao kwa ushirikiano na mwakilishi wa kata hiyo kwenye bunge la kaunti. Na hii sio natija ya pekee iliyopatikana kutokana na mabadiliko haya ya kisiasa. Kabla siku ya leo, ilimbidi mkazi yeyote wa Kijiji cha Kaulizeni ajiandae vyema kabla ya kuenda zahanatini kwa matibabu kwa **chamcha** kilicholiwa asubuhi au kupakiwa kwenye mifuko ya sandarusi kabla ya kupigwa marufuku na shirika linalodhibiti ubora wa mazingira maarufu kama NEMA, ili kiliwe huko ukisubiri kuhudumiwa. Ama kweli milolongo iliyopangwa kuingia katika kila sehemu hapo zahanatini ilikuwa mirefu: si pa usajili, si pa uchunguzi wa daktari, si pa malipo, si maabarani, si pa dawa na hata msalani foleni ilikuwapo si hoja kwamba uchafu uliokuwepo ulitosha kumfanya mja apoteze haja ya kuzuru huko ghafla.

Ilisemekana kwamba wafanyakazi wa hapo zahanatini ndio walisababisha chelewesho hili na kufanya foleni kurefuka katika kila idara. Mathalani, madaktari walisemekana kuingia kazini saa nne hivi baada ya kupitia kliniki zao za kibinafsi na kuondoka kabla ya saa tisa. Maafisa wa usajili nao walificha majalada maksudi ili kubembeleza kadhongo kutoka kwa wagonjwa kabla kuanzisha usajili wao. Wale wanaohusika na dawa walizoea kuwambia wagonjwa kuwa dawa zilikuwa zimeisha na kuwaelekeza kwenye maduka ya wauza dawa karibu sana na zahanati yenyewe. Halafu ukifika huko na kununua dawa, **unapigwa na butwaa** kuona dawa ulizouziwa zikiwa na nembo ya serikali. Hakika waso haya wana mji wao. Sikuelewa ni kwa nini udokozi wa namna hii ulifanywa hadharani mchana wa Mungu.

Kwenye maabara kulisemekana kwamba kemikali maalum za kutumiwa kupima maradhi hazikuweko hivi kwamba matokeo ya uchunguzi yalionyesha kwamba kila mgonjwa alikuwa na aina ileile ya ugonjwa. Maarufu miongoni mwa maradhi yaliyodhihirishwa maabarani ilikuwa malaria na homa ya matumbo. Sasa haikuwa ajabu mtu kutilia shaka uchunguzi uliofanywa katika maabara haya. Matokeo haya yalitolewa baada ya kipindi kirefu cha kusubiri kwa wastani saa mbili na nusu! Usishangae kwamba wakati wa kipindi hiki cha kusubiri, wangeonekana wakiwa katika harakati kama wahandisi wanaokarabati mtambo maalum wa tarakilishi mara wanakoroga, mara wanamimina majimaji vyomboni au wanakonyeza macho kutazama miujiza waliyotambua wao pekee yao kama wanajimu wanaozuru anga za juu. Wale wa idara ya malipo walikuwa maarufu kwa kuwambia wateja wao kwamba hawakuwa na hela za kuwarejeshea kama mabaki yao; wakawa na masalio ambayo, kama kawaida kidogo kidogo hujaza kibaba, yalizalisha maelfu ya pesa katika kipindi kifupi na kunenepesha mifuko yao.

Gavana wa gatuzi hili alifagilia mbali uchafu huu wote. Mori alihudumiwa katika kipindi cha chini ya saa moja baada ya ugonjwa wake kupatikana. Ugonjwa wake ulikuwa ni mwiba wa kujidunga ambapo mhasiriwa hastahili kuambiwa pole. Ukaidi wao uliwafanya kukataa kulala chini ya vyandalua vya kuwazuia wadudu wasababishao maradhi haya sugu kwa kuongozwa na imani potofu eti vyandarua huzuia usingizi. Usisahau kwamba vilitolewa bure kwa kila mkazi wa gatuzi hili kupitia mpango maalum wa rais wa taifa mojawapo la ulimwengu lenye ustawi mkubwa wa viwanda. La kuchekesha zaidi ni kuviona vyandarua walivyopewa vikiwa vimetumiwa kuzingira vitalu vilivyopandwa mboga. Hiki ndicho kinaya kilichozuliwa na Mori na mkewe hata wakawa windo rahisi kwa mbu.

Maswali

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

a) Orodhesha hoja **tatu** zinazoonyesha maendeleo yaliyotokana na ugatuzi kulingana na makala. (alama 3)

b) Kabla ya ugatuzi, wafanyakazi wa vituo vya afya walikuwa wanawanyanyasa wagonjwa. Taja makosa **matano** yaliyofanywa na wafanyakazi mbalimbali wa vituo vya afya. (alama 5)

c) Wataje viongozi **wawili** wa kuchaguliwa wanaozungumziwa na msimulizi. (alama 2)

d) Nakili neno moja kutoka **aya ya pili** lenye maana sawa na **plastiki**. (alama 1)

e) Taja jina la ugonjwa aliokuwa anaugua Mzee Mori. (alama 1)

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kifunguni. (alama 3)

   i) kuhujumu …………………………………………………………………………………….
   ii) chamcha ……………………………………………………………………………………
   iii) unapigwa na butwaa ………………………………………………………………………….

**2. Ufupisho (Alama 15)**

**Soma makala kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Kilimo ni moja kati ya shughuli muhimu sana zinazotekelezwa na binadamu katika vizazi vyote na hujishughulisha na upanzi wa mimea na ufugaji wa wanyama. Maisha ya binadamu katika nyanja zote hutegemea kilimo hivi kwamba endapo harakati za kilimo zitasitishwa, bila shaka maisha ya binadamu yatafikia kikomo. Chakula na mavazi ya binadamu hupatikana kutokana na shughuli hii muhimu na imekuwepo maishani mwa binadamu kwa karne nyingi. Wataalamu wa historia husema kwamba kilimo kilianza wakati ambapo ustaarabu wa binadamu ulianza kustawi yaani kadri binadamu alivyoanza kukumbatia ustaarabu ndivyo kilimo kilianza kustawi hali kadhalika. Kabla ya kustawi kwa kilimo, binadamu wa kwanza aliishi maisha ya kulumbata wanyama akikusanya miti, majani, maganda, mizizi na matunda kwa ajili ya kujikimu maishani mwake. Katika kipindi hiki mtindo huu wa kupata chakula na mavazi ya binadamu ulikuwa mwafaka mradi hakuweza kutindikiwa na chochote.

Baadaye dharura ya kuwa na utaratibu tegemevu wa kujipatia maslahi ya binadamu ikatokea kwa sababu ya kuendelea kuongezeka kwa idadi ya watu, pakawa na haja ya kulainisha mfumo wa uzalishaji wa chakula na kutimiza mahitaji mengine ya kibinadamu. Matokeo ya juhudi hizi yalianzisha shughuli ya uvuvi, uwindaji wa wanyama na ndege na usanyaji wa vyakula mbalimbali na kuvihifadhi. Harakati za kusaka chakula kwa wingi

zikashadidi katika kila janibu za ulimwengu. Hii ilifuatiwa na kuanza kufuga wanyama waliozalisha bidhaa kama vile maziwa, nyama, ngozi na mayoya yaliyotumiwa kutengeneza mavazi. Wanyama waliofugwa hivi, baada ya miongo fulani, wakaanza kutumiwa mashambani kufanya kazi ya kusaidia kuandaa mashamba kwa minajili ya kuzalisha vyakula.

Ustaarabu ulipoimarika zaidi kutokana na mpito wa wakati, mahitaji ya chakula kilichozalishwa kupitia kilimo yakawa makubwa kushinda chakula kilichokuwepo kwa ajili ya kuyakimu mahitaji ya binadamu katika kipindi hicho cha kizazi cha binadamu. Jambo hili lilisababisha haja ya kubuni mbinu mpya na bora zaidi za uzalishaji wa chakula kutokana na matumizi ya ardhi.

Aghalabu katika baadhi ya sehemu, uzalishaji ulizuiwa na hali ngumu ya hewa kwa sababu ya mvua isiyotegemewa, ama ichelewe au ipotee kabisa na kusababisha kiangazi kilichonyausha na kukausha mimea mashambani. Mimea mashambani inaachwa ikisononeka kutokana na uhaba au ukosefu kabisakabisa wa maji. Ili kukabiliana na changamoto hii ya hali ya hewa, mitaro mikubwa ilichimbwa kutoka maeneo ya maji kama vile mabwawa, mito ya kudumu, maziwa na vidimbwi ili kuelekeza maji mashambani na kuwezesha mimea kustawi ipandwapo. Huu ulikuwa mwanzo wa kilimo cha kunyunyizia maji mashambani. Mtindo huu ulistawi zaidi nchini Misri Kaskazini mwa Bara la Afrika kwa sababu ya kuwepo kwa Jito la Nile. Mbali na kutumia mtindo wa kunyunyizia maji mashambani ili kuimarisha uzalishaji, haja ilizuka ya kuimarisha aina ya mbegu zilizopandwa ili kuongeza kiwango cha mazao ambayo yangepatikana hata katika eneo dogo. Kadhalika, mbegu zilizoimarishwa hivi zilikuwa na uwezo wa kuhimili hali ngumu ya hewa kama kiangazi, magonjwa na wadudu waharibifu. Hizi zilikuwa baadhi ya hatari zilizokumba mimea na kudunisha kiwango cha mazao yanayotoka kwenye mashamba. uzalishaji.

Usisahau kwamba uvumbuzi wa viwanda ulipozuka kule Ulaya, vifaa bora vya kutumia katika kilimo vilivumbuliwa. Vifaa hivi vilikuwa kama vile plau na tingatinga na vilisaidia sana kuandaa konde kwa njia bora zaidi na tena kwa kipindi kifupi. Hatua hii iliimarisha mchakato mzima wa kuendeleza kilimo kwa manufaa ya binadamu. Kwa kweli akili ni mali na si mali tu bali ni mali ya aina yake. Ni dhahiri kwamba mti hauwezi ukaenda pasipo na nyenzo.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

a) Fupisha **aya mbili za kwanza** ukitumia kati ya 70 na 80. (alama 6)
**Matayarisho**
**Nakala Safi**

b) Kwa maneno 80 hadi 90 andika hoja muhimu katika aya ya **tatu na ya nne**. (alama 9)
**Matayarisho**
**Nakala Safi**

**3. Matumizi ya Lugha (Alama 40)**

a) Taja na ainisha konsonanti zilizo katika neno **'ng'ata'** ukizingatia ala za kutamkia. (alama 1)

b) Toa mifano **minne** ya maneno yenye irabu tatu pekee katika Kiswahili sanifu. (alama 2)

c) Onyesha silabi zenye kutiliwa mkazo wakati wa kutamka maneno yafuatayo: (alama 1)
i. ombea …………………………………………  ii. hakimu ……………………………

d) Eleza maana **mbili** tofauti katika sentensi: (alama 2)
Dumu na mwanawe Bor ni waimbaji hodari.

e) Tunga sentensi **mojamoja** ukitumia kivumishi cha pekee **- ingineo** ukianza kwa maneno yafuatayo: (alama 3)
i) sisimizi:
ii) mkanda:
iii) kuchoka:

f) Andika muundo wa sentensi hii kwa kutumia msitari. (alama 2)
Mgogoro huo ulimalizika leo kwa mapatano.

g) Ainisha mofimu katika neno **'iue'**. (alama 2)

h) Onyesha kisha uainishe nomino katika sentensi hii: (alama 3)
Kipakatalishi cha Wangila kina kasi kubwa.

i) Akifisha sentensi hii: (alama 3)
umeanza kusoma tamthilia ya kigogo kigogo alimuuliza kangogo.

j) Kanusha:
i) Wanafunzi wengi wameenda kucheza kandanda katika shule jirani. (alama 1)
ii) Tukianza safari yetu asubuhi tutachelewa kikaoni. (alama 2)

k) Andika kwa kinyume:
Wananchi wengi walihudhuria mkutano ndani ya uga wa Kitaifa. (alama 2)

l) Geuza katika umoja au wingi kulingana na maagizo ndani ya mabano mwishoni mwa kila sentensi.
i) Idara mpya iliundwa na mkurugenzi wa kampuni hiyo. (wingi) (alama 1)
ii) Vyungu vya kupikia vimesahaulika na wapishi. (umoja) (alama 1)

m) Tunga sentensi zilizo na miundo ifuatayo:
i) S - KN (W+V) + KT (T+E) (alama 2)
ii) S - KN (N)+ KT (T) (alama 1)

n) Andika sentensi hii ukitumia maneno yenye maana sawa na yale yaliyopigiwa mistari. (alama 2)
<u>Banati</u> <u>alishusha</u> <u>beramu</u> saa <u>kumi na mbili</u> jioni.

o) Kwa kutumia sentensi **moja**, tofautisha vitate vifuatavyo: **sima, zima** (alama 2)

p) Ni methali gani inayolengwa na maelezo yafuatayo? (alama 2)
Panapokuwa na juhudi katika jambo lolote hata likiwa gumu, hatimaye ufanisi hupatikana.

q) Tumia nahau '**ng'oa nanga**' katika sentensi ili kudhihirisha maana yake. (alama 1)
(alama 2)

r) Jaza pengo kwa vihisishi mwafaka. (alama 3)
Unapotaka kupishwa hutumia neno ………………………………. na ………………………..
ni tamko la kuagana mnapoachana na mtu usiku kama ambavyo …………………………….
hutumiwa unapomwomba mtu msamaha kwa kumkosea.

**4. Isimujamii (Alama 10)**
Andika sifa **kumi** za lugha utakayotumia ukipata fursa kutangaza mchezo wa kandanda. (alama 10)

**MTIHANI WA MWIGO WA SUKELLEMO**
**102/3**
**KISWAHILI KARATASI YA 3**
**LUGHA** access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU A :CHOZI LA HERI**
**Assumpta K. Matei : Chozi la heri**
**SWALI LA LAZIMA**
**1..** "Vipi, binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika?"
**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
**b)** Tambua mbinu ya lugha iliyotumika. (alama 2)
**c)** Jadili sifa tatu za msemaji. (alama 3)
**d)** Hakiki jinsi binadamu alivyomwagikiwa na maji katika riwaya (alama 11)

**SEHEMU B : TUMBO LISILOSHIBA**
**Jibu swali la 2 au 3**
**2. Shibe inatumaliza : Salma Omar Hamad**
"Hiyo ni dharau ndugu yangu. Kwa nini kila siku tunakula sisi kwa niaba ya wengine ?"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza jinsi jazanda inavyojitokeza katika hadithi. (alama 4)
c) Eleza sifa za msemaji. (alama 4)
d) Eleza jinsi viongozi wanavyokuwa wabadhirifu. (alama 10)

**3. Mwalimu Mstaafu:Dumu Kayanda**
"Sijawahi kusema kwenye kipaza sauti tangu nizaliwe."
a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Eleza umuhimu wa hotuba ya mzungumzaji katika dondoo hili. (alama 10)
c) Onyesha jinsi suala la usaliti linavyojitokeza katika hadithi ambamo kauli hii imetolewa.(alama 6)

**SEHEMU C: KIGOGO Pauline Kea**

**Jibu swali la 4 au 5**

**4**. ”Hayatapoa…kumewaka na kutateketea tusipouzima moto.Liwalo na liwe!”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Bainisha vipengele viwili vya kimtindo vinavyojitokeza katika dondoo hili. (alama 3)

c) Tathmini umuhimu wa anayeambiwa maneno haya katika tamthlia. (alama 5)

d) Onyesha jinsi mzungumzaji alivyouzima moto uliokuwa umewaka jimboni Sagamoyo. (alama 8)

**5**. Jadili nafasi ya Wanasagamoyo katika kudorora kwa maendeleo ya jamii yao. (alama 20)

**SEHEMU D:USHAIRI**

**Jibu swali 6 au 7**

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Hizi bombo mwaanika, wa ndizini nashtuka,
Peupe mwazianika, kwenye jua kukauka,
Zingine zimeraruka, aibu zinatufika,
Anikeni kwa kuficha, za ndani mkisafisha.

Nako kule kwenye bafu, mwaziweka hizo chafu,
Hilo nalo nakashifu, mkitoa nitasifu,
Kuziweka maji chafu, hilo ndilo ninahofu,
Anikeni kwa kuficha, za ndani mkisafisha.

Kwenye meza wazileta, wana wenu wakipata,
Wageni wakijateta, aibu haitatupata?
Muondoeni utata, hizo zenu twazipata,
Anikeni kwa kuficha, za ndani mkisafisha.
Kwa heshima tudumuni, tufaapo za mwilini,
Tamaduni jifunzeni, msiige uzunguni,
Za bafuni zi jikoni, zi watoto makononi,
Anikeni kwa kuficha, za ndani mkisafisha.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Wino wangu kibindoni, nitatua tamatini,
Za ndani ziwe za ndani,msonyeshe hadharani,
Za bafuni si jikono, msiweke kabatini,
Anikeni kwa kuficha, za ndani mkisafisha.

**<u>MASWALI</u>**

a) Pendekeza kichwa mwafaka katika shairi hili. (alama 1)

b) Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)

c) Tambua nafsineni katika shairi. (alama 1)

d) Jadili matumizi ya mitindo ifuatayo ya lugha katika shairi hili.

  i) Kinaya (alama 2)

  ii) Usambamba (alama 2)

  iii) Balagha (alama 1)

e) Onyesha kuwepo kwa uhuru ufuatao katika shairi. (alama 3)

  i) Tabdila

  ii) Kubananga sarufi

  iii) Inkisari

f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha mjazo. (alama 4)

g) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 5)

**7. YALIMWAGIKA**

Lilianza kama wazo, nikawaza,
Niwe na watoto,
Si vikwazo, ghafla mama yao akapatikana,
Kwa rutuba yake,
Akavimba
Kumbe ni mapacha,
furaha!

Majina walishapewa,
Imani kudumu, watazaliwa,
Tungo wakatungiwa,
Amani na Imani,
Baba yao ni malenga
Anatayeita maneno.
Maneno yanaitika.
Nikasubiri.

Wazazi walitamani kupakata,
Amani na Imani
Iwe yao burudani, siyo kama zamani
Wachezee zuliani.
Baba niwaweke kifuani
Na migongoni bila susu, kwa mama yao
Si mtoto hutizama kisogo cha ninake?
Tukangoja!

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com
Furaha kote nyumbani iliwatanda,
Kuyaona makinda yao, kwa kitanda,
Wadondokwe udende, wawapende!
Mama anyonyeshe, kiwatazama machoni,
Kuwagusa mashavuni, waliapo.
Watulie Amani na Imani.

Ukutani ni kiwimbo, baba alishawatungia,
Kushotoni ni wa kike, kuumeni kijanadume
Watulie, Baba yao aliwazia
Wazo likaanza kupokwa.
Hospitali wakiwasili.

Wiki zikajenga miezi
Tamati ikajongea
Kawanunulia mavazi
Walifaa kuvaa
Hawakuvaa!
Vijulanga miezi saba, pukachaka!
Kifo ni mwewe, kikaninyakulia.
Amani na Imani.
Tunalia!
Pema peponi wanetu!

**MASWALI**

a) Eleza jinsi usimulizi ulivyotumika kwenye shairi. (alama 1)
b) Eleza sifa tatu zinazoafiki shairi hili kuwa huru. (alama 3)
c) Shairi hili ni la tanzia. Thibitisha. (alama 1)
d) Tambua mandhari ta tanzia. (alama 1)
e) Tambua nafsineni kwenye ubeti wa kwanza. (alama 1)
f) Eleza toni ya shairi. (alama 2)
g) Onyesha mifano miwili ya matumizi ya sadfa katika shairi. (alama 3)
h) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha tutumbi. (alama 4)
i) Eleza maana ya msamiati huu kulingana na shairi. (alama 4)
   i) Vijulanga
   ii) Susu
   iii) Akavimba
   iv) ..Kiwimbo

**SEHEMU E:FASIHI SIMULIZI**

**8** a) Eleza jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza fasihi simulizi. (alama 5)
b) Fafanua matatizo yanayomkabili mkusanyaji wa fasihi simulizi nyanjani. (alama 10)
c) Eleza umuhimu wa ukusanyaji na uhifadhi wa data za fasihi simulizi. (alama 5)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

–
–
–
–

–
–
–
–
–

–
–
–

**KIRINYAGA WEST**
**JARIBIO LA TATHMINI LA PAMOJA KIDATO CHA NNE - 2021**
**102/1**
**KISWAHILI KARATASI 1 (INSHA)**
**DECEMBA 2021**
**KIDATO CHA NNE**

1. **Swali la lazima.**
   Wewe ni mhariri wa Gazeti la Mwanzo Mpya, andika tahariri kuhusu juhudi ya serikali kuimarisha sekta ya elimu nchini Kenya. (alama 20)

2. Kukaa nyumbani kwa muda mrefu sana bila kwenda shuleni kulileta athari mbaya kwa wanafunzi. Eleza. (alama 20)

3. Andika kisa kitakachothibitisha maana ya methali ifuatayo:-
   Usitukane wakunga na uzazi ungalipo. (alama 20)

4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
   Nilitoa simu yangu mfukoni na kuipokea bila kuangalia ni nani alikuwa akinipigia. Nilipoipokea ilinidondoka ....... (alama 20)

**KIRINYAGA WEST**
**JARIBIO LA TATHMINI LA PAMOJA KIDATO CHA NNE - 2021**
**102/2**
**KISWAHILI KARATASI 2 (Ufahamu, Ufupisho, Sarufi na Isimu Jamii)**
**DESEMBA 2021**

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

1. **UFAHAMU**.(alama 15)
   **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Ulikuwa usiku wa manane, mavia hatawahi kuyasau yaliyotokea usiku huo na madhara yaliyoikumba aila yake; ambayo hadi wa leo huwasumbua na kuwafuata kila waendako na hata kuishi. Matokeo ya kitendo kilichotekelezwa na nduguye Mnuna yamesalia kama dondandugu moyoni mwake. Yeye hujaribu kuyafutilia mbali lakini yanakataa katakata kuondoka fuvuni mwake hasa anapomtazama nduguyue mdogo. Maria alikuwa akidurusu somo la Fizikia. Abdalla kakake mkubwa akimpa Tom wosia. "Tom, itakuwa bora ikiwa mtanena kwa amani na baba kuhusu tofauti zenu."

Hamna haja ya kumrushia cheche za matusi, kumbuka kuwa heshima kwa mzazi ni taadhima kwa mterehemezi matokeo yake ni baraka na sudi tele." Tom alikinai kuyatilia maanani mawaidha ya kaka yake. Akajitia hamnazo na kudai kuwa baba yake amemdunisha kwa muda mrefu na angemfunza adabu. Watu wote katika familia walijaribu kumsihi lakini ikawa bure.

"Upyaro haufai ndugu yangu. Hata kama una kimo kikubwa kuliko baba kumbuka kuwa ndiye mzazi aliyekulea wewe." Alidokeza Maria.

Baba yake Maria, Mugambi, alikuwa amechoshwa na vitendo vya mwanawe vya kutumia dawa za kulevya. Aghalabu Tom alikuwa akizua rabsha kila jioni baada ya kutoka shule. Mugambi alikuwa amemwadhibu mwanawe na hata kumshtaki katika kituo cha polisi lakini hakubadilika. Watu walisema kuwa alikuwa na fedha nyingi kutokana na ulanguzi wa mihadarati. Jambo hili humwezesha kuhepa mitego ya askari kwa <u>kuzunguka mbuyu</u>. Tom akawa asiyesikia la mwadhini wala mteka maji msikitini.

"Mzee ninataka unipe urithi wangu, la sivyo leo utaiona dunia hii paa!" Tom akamtisha baba yake. Mugambi akaja juu na kumwambia mwanawe kuwa umri wake haukutosha kupewa urithi. Ingembidi akamilishe masomo kwanza ajijengee msingi bora wa maisha yake ya kesho na hata kupata mali yake mwenyewe." Mimi si mtoto. Ninataka uelewe kuwa leo ikiwa siku yangu ya mwisho kuhudhuria shule. Hiyo elimu ya wakoloni imenichosha! Katu sisomi tena." akasema Tom. Punde si punde Mugambi alipandwa na za mkizi na kumwandama mwanawe

kwa makonde ikawa vurugu si vurugu. Kuwamamanua bila mafanikio. Licha ya kuumizwa na kujeruhiwa sehemu kadha za mwili wake, Tom alishikilia kikiki na kuendelea kupambana na baba yake. Mama yake alipoona maji yamezidi unga, aliamua kuingilia kati na liwe liwalo kwa bahati mbaya Tom alimrushia teke la ubavuni wake na kumwangusha chini pu!

"Aghrr! Haya yote unayotufanyia sisi wazazi wako yatakufuata daima." Mugambi alilaani huku akigaragara sakafuni kwa maumivu tele. "Ninataka uniuwe leo, siwezi kukulea mwa dhiki na taabu tele halafu unikosee mimi na mamako heshima namna hii utaona kilichomtoa kanga manyoya," Mugambi alimwambia mwanawe akiwa na uchungu mwingi moyoni. Majirani mimi nikiwemo walikuja kujionea sinema ya bure: "Teresia, unaona namna Tom alivyowakosea wazazi wangu heshima?" Maria aliniuliza kwa muda mrefu familia yetu imekosa amani kwa sababu ya Tom kuzua fujo mara kwa mara. Amewajeruhi wazazi wangu mara nyingi huku akivivunjavunja kenyekenye vyombo vya mama. Tandabelua anaozua Tom hunifanya mimi na ndugu zangu kutohudhuria shule wakati mwingine. Huwa tunahofia kuangamizwa kwa wazazi wetu, hivyo kubaki nyumbani kama walinzi wao. Tom amegeuka hayawani. Hajali habali." alinieleza Maria huku machozi yakimtiririka tiriri, njia mbili mbili.

Nyumba yetu ilikuwa mita chache kutoka nyumbani kwa akina Maria. Nilikuwa wa kwanza kushuhudia Tom akiwatendea wazazi wake unyama pamoja na ndugu yake Abdallah. Alikuwa amewajeruhi vibaya. Abdallah alipojaribu kuwasaidia wavyele wake alirushiwa upanga uliompata barabara kwenye kisigino. Ninakumbuka namna Abdallah alivyochechemea kwa uchungu mwingi huku akiwa ameyauma meno. Ninakumbuka vyema. Kama wote walioshuhudia unyama wa Tom walilengwalengwa na machozi huku wakiulaani. Wanakijiji cha umoja waliamua kumpiga kitutu na kumfukuza. Alipotambua wamemzidi nguvu, alikimbia kiswara na kuelekea upande wa chini. Kwa bahati mbaya, alianguka shimoni na kuvunjika miguu yote miwili. Aketipo na kudhukuru vitendo alivyokuwa akiifanyia familia yake Tom hupatwa na majuto makubwa. Leo ameamini kuwa majuto ni mjukuu.

**Maswali.**

(a) Eleza msimamo wa Mugambi kuhusu kumpa mwanawe urithi. (alama 2)

(b) Taja sababu kuu iliyomfanya Tom kutekeleza vitendo vya kinyama. (alama 1)

(c) Kwa kurejelea kifungu, thibitisha jinsi uozo ulivyokithiri katika jamii ya umoja. (alama 4)

(d) Fafanua wasifu wa Tom kulingana na taarifa hii. (alama 2)

(e) Eleza suala la uwajibikaji kama linavyojitokeza katika taarifa. (alama 3)
Access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)
- (i) sudi
- (ii) kuzunguka mbuyu
- (iii) kuwamamanua

2. **UFUPISHO (alama 15)**
**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Serikari kupitia wizara ya Elimu imetoa mwongozo wa karo ambao unastahili kuzingatiwa katika shule za upili kufuatia hatua ya shule mbalimbali kuongeza karo kwa viwango mbalimbali. Hatua hiyo inadhamiriwa kumkinga mzazi dhidi ya kunyanyaswa kifedha hasa ikizingatiwa kuwa gharama ya maisha imepanda mara dufu. Hata hivyo ingekuwa bora ikiwa serikali ingefanya maamuzi kwa ushirikiano na walimu wakuu maana kwa hakika suala la karo linahusu matumizi ya fedha ambayo pia huja na gharama zake. Gharama hii inatokana na ununuzi wa vitabu vya kiada na vya mazoezi, karatasi za uchapishaji mitihani, kwa kuwa wanafunzi sharti wasome na waandike.

Vilevile, gharama hii inatokana na ununuzi wa kemikali za kutumiwa katika maabara. Aidha, kuna gharama ya kuendesha michezo na tamasha za muziki na drama. Wanafunzi wa shule za malazi hula na kulala na kwa sababu hiyo maamuzi ya kifedha lazima yafanywe.

Jambo ambalo linastahili kuangaliwa kwa makini ni viwango vya kupanda kwa gharama ya maisha. Lazima tujiulize gharama hiyo imepanda kwa kiasi gani na wapi? Kwa kweli haiwezekani kununua kilo moja ya mahindi kwa bei hiyo hiyo Kitale, Mombasa na Turkana. Vile vile ni muhimu kujiuliza ikiwa shule husika ni ya mashambani au ya mjini? Kwa hivyo, sharti la kifedha ni muhimu katika kuamua karo ya shule na maeneo mbalimbali nchini.

Pili, hebu tuangalie ikiwa shule inayohusika ni ya kiwango cha kaunti ndogo, kaunti au cha kitaifa. Hii ni muhimu kwa kuwa hali ya masomo katika shule hizo hutofautiana. Tofauti kuu hutokana na miundomisingi na programu za masomo zinazoendeshwa. Kwa mfano, programu za kutathmini, kompyuta na zinazohusu ziara huhitaji fedha nyingi. Shule ambayo ina masomo kama vile muziki, sanaa na sayansikimu sharti zitoze karo ya juu kwa kuwa masomo hayo huandamana na gharama ya kununua vyombo na vyakula? Sasa mbona fedha za

ziada? Wanaotetea kupunguzwa kwa karo wanapunguza mchango wa motisha katika ufanifu wa masomo. Ndio, baadhi ya shule hutoza karo ya juu ili kuwamotisha walimu kwa vyakula na kwa zawadi ili kuwastahi wanapopata matokeo mema. Hali hivyo huwafanya kujikakamua kazini na kutoa hduma ya hali ya juu.

Fedha za ziada vile vile hutumiwa kuwaajiri walimu wa ziada ikizingatiwa kuwa serikali haijawaajiri walimu wa kutosha. Pia katika baadhi ya shule, wanafunzi huandaliwa vyakula spesheli tofauti na mseto wa maharagwe na mahindi almarufu 'maram' uliozoeleka katika shule nyingi. Ikumbukwe kuwa lishe bora ni mojawapo ya haki za kimsingi kwa watoto ambayo sharti iheshimiwe. Kwa marefu na mafupi yake, serikari haipaswi kuweka viwango sawa vya karo kwa kila shule kwa maana hilo huenda likazua mgogoro wa kiutawala katika shule nyingi. Shinikizo za kupunguzwa kwa karo inayotozwa hasa katika shule za upili zinafaa kutetewa kimantiki wala si kihisia.

Mambo huenda yangekuwa tofauti ikiwa serikali ingewajibika kwa upande wake kwa kuwaajiri walimu wa kutosha kuwaongeza walimu mshahara na kuwatambua kwa zawadi wanapofanya kazi nzuri na kuwapandisha vyeo. Hata hivyo, mgala muue na haki umpe; hatua kali zinapaswa kuchukuliwa dhid ya walimu wanaowatoza wazazi karo ya juu kupindukia ili kuendeleza maslahi yao ya kibinafsi.

Naamini kuwa hatua ya waziri wa Elimu kukutana na washikadau katika sekta ya Elimu kuhusu karo na uteuzi wa wanafunzi wa kujiunga na shule za upili ni ya busara na inafaa kutoa mwelekeo mzuri kuhusu masuala tata yalivyopo kwa sasa.

**Maswali.**

(a) Fafanua mambo muhimu yanayostahili kuzingatiwa katika kutathimini viwango vya karo katika shule nchini Kenya. (maneno 65 - 70) (alama 8, 1 ya mtiririko)
Nakala chafu
Nakala safi

(b) Fupisha aya tatu za mwisho. (maneno 40 - 45) (alama 7, 1 utiririko)Nakala chafu
Nakala safi

3. **MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 40)

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

(a) Andika maneno yenye miundo ifuatayo:- (alama 2)
 (i) Kipasuo ghuna cha mdomoni, irabu ya chini kati, kitambaza cha ufizini, irabu ya mbele juu
 (ii) Irabu ya nyuma juu, irabu ya nyuma kati, kikwamizo ghuna cha mdomo meno, irabu ya nyuma juu

(b) Andika neno lenye muundo ufuatao:- (alama 1)
KIIKI

(c) Bainisha silabi inayowekwa shadda katika neno lifuatalo. (alama 1)
Nyumba

(d) Tumia nomino yoyote katika ngeli ya u - u kutunga sentensi. (alama 1)

(e) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali ya kuendelea :- (alama 2)
Mtihani ulitungwa na jopo la watahini

(f) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo.
 (i) Wanafunzi <u>walisoma</u> ili <u>kuzifaidi</u> familia zao.
 (Badilisha vitenzi viliyopigwa mstari kuwa nomino) (alama 1)
 (ii) Asingalikuwa na gari asingalifika mapema. (Yakinisha katika wingi) (alama 1)
 (iii) Mkulima huyu atalima shamba hii (Anza kwa: Shamba .....) (alama 1)

(g) Andika katika usemi halisi. (alama 2)
Mwajiri aliwaonya wafanyakazi wake waache uzembe kazini.

(h) Tunga sentensi ukutumia kitenzi -la katika kauli ya kutendesha. (alama 2)

(i) Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha matumizi ya mshazari. (alama 2)

(j) Bainisha virai katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Waziri wa elimu alifanyisha kazi haraka sana.

(k) Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia 'O' rejeshi tamati . (alama 2)
 Mlango ambao utafungwa ni huu.

(L) Tunga sentensi ukitumia kiambishi 'na' kuleta dhana ya wakati. (alama 1)

(m) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mvua itakapopusa tutaondoka mara moja.

(n) Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo:- (alama 3)
Vibarua wamemfanyia tajiri kazi haraka ipasavyo.

(o) Andika katika udogo. (alama 1)

Nguo iliyonunuliwa imeoshwa

(p) Changanua sentensi zifuatazo kwa mitindo iliyobanwa.
   (i) Mtihani ulifanywa tulipokuwa ziarani (matawi) (alama 2)
   (ii) Mpe vitabu vyake vyote (mstari) (alama 2)

(q) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha dhana ya uteuzi. (alama 2)

(r) Tunga sentensi mbili kudhihirisha maana tofauti za neno jua. (alama 2)

(s) Eupe ni kwa ensi ____________ ni kwa embamba na _________________ ni kwa levuka. (alama 1)

(t) Tumia kivumishi ha idadi jumla pamoja na nomino katika ngeli ya KI-VI kutunga sentensi. (alama 2)

(u) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya: (alama 2)
ndoa
doa

4. **ISIMU JAMII.** (alama 10)
Kwa kutumia mifano mwafaka eleza jinsi kaida zifuatazo zinavyoathiri matumizi ya lugha.

(a) Mazingira (alama 3)
(b) Taaluma (alama 2)
(c) Umri (alama 3)
(d) Malezi (alama 2)

**KIRINYAGA WEST**
**102/3**
**KISWAHILI KARATASI 3**
**FASIHI**
**DESEMBA 2021**

**SEHEMU A: USHAIRI**

1. **Swali la lazima.**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Naja sasa ni ndiyani, naja kwetu mzalendo,
Naja nirudi nyumbani, nilowekwa nako kando,
Kwetu 'mi nakutamani, kulo na mwingi uhondo,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

Naja kwingine kuwapi, kulojaa langu pendo?
Huenda nende kwinginepi, sawa nako kwa muundo?
Kaa kwingine anapi, ela kwenye lakwe gando?
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

Naja nije rudi papo, panigedeme mgando,
Ningaambwa kwetu hapo, kwamba kwanuka uvundo,
Sitakwenda penginepo, tarudi huko kwa mwando,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

Naja sitapakimbiya, ningambwa kuna vimondo,
'Takuja kuvilekeya, vinganijiya kwa vundo,
Nilipozawa tafiya, sikimbii kwenda kando,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

Naja hiwa 'mekomaa, kuzidi nilivyo mwando,
Tena n'najiandaa, kwa fikira na vitendo,
Kwetu nije kuifaa, na kuitiliya pondo,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

Naja na ingawa naja, siwaeki mifundo,
Moyo wangu ushatuja, mawi nalotendwa mwando,
Ela wataoningoja, na vyao viwi vitendo,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

**Maswali**

(a) Kwa kudokeza hoja **nne**, bainisha uzalendo wa mshairi katika ubeti wa 1 na 2. (alama 2)
(b) Eleza bahari zinazojitokeza katika ushairi huu kwa kuzingatia:- (alama 3)
  (i) Mpangilio wa maneno.
  (ii) Idadi ya pande
  (iii) Mpangilio wa vina katika beti.
(c) Bainisha umuhimu wa maswali ya balagha katika shairi hili. (alama 2)
(d) Eleza toni ya mshairi. (alama 1)
(e) Bainisha aina **mbili** za urudiaji katika shairi hili. (alama 2)
(f) Eleza umuhimu wa idhini ya kishairi uliotumika katika shairi hili. (alama 4)
(g) Bainisha sifa mbili za kiarudhi zinazojikita katika ubeti wa pili kutoka mwisho. (alama 2)
(h) Andika ubeti wa tatu katika lugha tutumbi. (alama 4)

**SEHEMU B: RIWAYA**
**Assumpta K. Matei: Chozi la Heri.**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. "Hili lilimtia ...... uchungu, akajiona kama aliyedhalilishwa na mwanamke"
  (a) Eleza maktadha wa dondoo hii. (alama 4)
  (b) Bainisha maudhui yanayoendelezwa katika dondoo hili. (alama 1)
  (c) Kwa kudondoa hoja **kumi na tano**, eleza namna maudhui uliyoyataja hapo juu yamejitokeza riwayani. (alama 15)

Au

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

3. " .... ng'ombe akivunjikia mguu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa."
  (a) Fafanua umuhimu wa mzungumzaji wa kauli hii. (alama 4)
  (b) Kwa kulejelea riwaya, onyesha jinsi wahusika wafuatao wanavyokuwa "ng'ombe aliyevunjikia mguu malishoni."
    (i) Kairu (alama 6)
    (ii) Pete (alama 6)
    (iii)Lemi (alama 4)

**SEHEMU C : TAMTHILIA - PAULINE KEA**
**KIGOGO**
**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Nenda basi, usinipandishe mori! sitaki hizo siasa za kitoto."
  (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  (b) Tambua vipengele viwili vya kimtindo katika dondoo hili. (alama 2)
  (c) Eleza jinsi msemaji anavyoendeleza vipengele vifuatavyo katika tamthilia.
    (i) Maudhui (alama 7)
    (ii) Ploti (alama 7)

au

5. "Damu ni mbaya mwanangu. Imemwagika nyingi sagamoyo. Ardhi imeingia najisi, inateketea.
  (a) Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya msemaji na msemewa katika kuijenga tamthilia ya Kigogo. (alama 10)
  (b) Jadili mchango wa vyombo vya dola katika hali ya maisha Sagamoyo. (alama 10)

**SEHEMU D : HADITHI FUPI**

**Jibu swali la 6 au la 7**

**Alifa Chokocho na D. Kayanda : Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.**

6. **Ndoto ya mashaka: Ali Abdulla Ali.**

"... Sasa nimechoka mja. Nimechoka hata naradua kufa kuliko kuishi."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. (alama 2)

(c) Kwa kudokeza hoja kumi na nne, bainisha kwa bayana kuwa mzungumzaji alikuwa na haki ya kuradua kufa. (alama 14)

au

**Mame Bakari: Muhammed Khelef Ghassany.**

7. " ....... hapo tena ilimjia ile picha chafu ambayo haijambanduka mpaka leo wakati ule ilipoanza. Aliendelea kuliona lile janadume asilolijua likimvamia na kumbaka ghafla. Kisha likambamiza ardhini na ardhi ikashuhudia ukatili na udhalimu ule. Hadi sasa masikioni mwake anaisikia miguno na mingurumo ya lile dubwana la janadume. Anahisi mpaka sasa kule kupapatuliwa na kujipapatua yeye mwenyewe. Hadi sasa pua yake imejaa ile harufu kali ya kutuzi iliyompa kipalizi na kumkohoza. Anahisi mno ule mdidimizo na mkandamizo wa kiwiliwili chake ..."

(a) Tambua aina tano za taswira kwenye dondoo hili. (alama 5)

(b) Bainisha vipengele vitano vya kimtindo kwenye dondoo hili. (alama 5)

(c) Onyesha suala la unyonge linavyoshughulikiwa katika hadithi hii. (alama 10)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8. **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Ewe kilizi
Ulozowea kujificha
nyuma ya mama kujikinga, dhidi ya milio
ya radi ilo juu mbinguni,
jua kesho ni siku ya siku,
Siku ya kujua mbichi na mbivu
Kutofautisha jogoo na vipora.

access free learning material by visiting www.freekcsepastpapers.com

Ngariba takaposhika kijembe
ndipo utakapojua bayani
ukoo wetu si wa kunguru
ikiwa hu tayari,
Sithubutu kamwe, wanjani kuingia,
Sije kuniaibisha miye, amiyo na akraba nzima.

**Maswali.**

(a) (i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 2)

(ii) Andika sifa mbili za jamii inayosawiriwa na utungo huu. (alama 2)

(iii) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika utungo huu. (alama 2)

(b) Fafajua majukumu saba ya kipera hiki katika jamii yako. (alama 7)

(c) Umepewa jukumu la kutafiti kuhusu utungo huu katika jamii yako. Eleza umuhimu wa kushiriki wakati wa utafiti. (alama 7)